Nipashe
Alhamisi Oktoba 22, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580376
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

FURSA
Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti
Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi
Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania
Namba : +255716500500
Barua Pepe: circulation@guardian.co.tz
Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020

**MAGUFULI** aahidi kufufua viwanda vilivyotelekezwa

UKURASA 2



**LISSU** sasa ageukia kuimarisha uchumi

UKURASA 2

# Vilio kila kona viapo mawakala




**NEC** yaongeza muda zaidi, wengine wapoteza maisha wakienda kuapishwa... *Endelea Uk. 2 & 4*



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli akizungumza na Mwenyekiti wa Chama cha TLP, Augustine Mrema, baada ya kumvalisha kofia ya CCM, eneo la Himo, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: IKULU**

# Viongozi dini watoa msimamo uchaguzi

UKURASA 3

## Maalim Seif atoa sharti kukubali matokeo

UKURASA 3

**MICHEZO** **MAKOCHA SIMBA, YANGA WATEMA 'UPUPU' LIGI KUU** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Tundu Lissu sasa aahidi kuimarisha uchumi

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MGOMBEA urais, Tundu Lissu (CHADEMA), amesema Watanzania wakimpa ridhaa ya kuongoza nchi, atahakikisha anaimarisha uchumi kwa kuondoa sheria kandamizi na kutengeneza miundombinu mizuri kwa wafanyabiashara.

Akizungumza na wananchi wa majimbo ya Bumbuli, Korogwe Mjini, Korogwe Vijijini, Muheza na Tanga mkoani Tanga jana, Lissu alisema akichaguliwa, atahakikisha anaimarisha uchumi wa watu ili kuwa na taifa lenye watu wenye uchumi mkubwa.

Alisema akiingia madarakani, atafuta vitambulisho vya mjasiriamali vinavyotolewa na serikali kwa wafanyabiashara wadogo.

"Hivi mnavyoviita vitambulisho vya mfanyabiashara kwangu mimi hapana, mtafanya biashara zenu kwa uhuru kama ilani ya chama chetu inavyosema 'Uhuru, Haki na Maendeleo ya Watu'," Lissu aliahidi.

Mtaalamu huyo wa sheria alisema, kilio kikubwa cha wananchi ni ugumu wa maisha, akiahidi kuwa katika uongozi wake jambo hilo litakuwa historia.

"Tumezunguka nchi nzima na kote tulikoenda, kilio kikubwa cha Watanzania ni ugumu wa maisha, maji, barabara, ajira na kero nyingine nyingi sana, nichagueni niende nikaondoe kero hizi na mateso mliyoyapata kwa miaka hii yote," alisema.

Kuhusu sekta ya maji, Lissu alisema atahakikisha kero hiyo inaondoka kwa kujenga miundombinu ya maji nchi nzima. "Haiwezekani mnakaa hapa kwenye milima na maji yanatiririka hayajulikani yanaenda wapi, Mkoa wa Tanga una vyanzo vingi vya maji lakini hakuna udhibiti, mimi nitaondoa kero hizi zote," Lissu alitamba. Kuhusu ahadi yake ya haki kwa wananchi, Lissu alisema atalinda haki, uhuru na maendeleo kwa watu wote kwa kufuata misingi ya sheria na katiba mpya.

"Mimi nitakuwa Rais wa haki kwa kuondoa dhuruma kwa Watanzania wote, uwe ni mkulima, mfugaji, mfanyabiashara, mfanyakazi wa umma na binafsi, wote mtapata haki zenu," aliahidi.

Katika kampeni zake hizo, Lissu pia aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi kupiga kura Jumatano ijayo ili kutumia haki yao hiyo ya kikatiba.

"Mjitokeze kwa wingi kupiga kura ambayo itatoa hatima ya taifa letu, kura ambayo itatoa haki, uhuru na maendeleo ya watu, mkikosea mtaendelea kuteseka sana, mtaendelea kukosa haki zenu," alisema.

Lissu pia aliitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha inatenda haki kwa vyama vyote katika uchaguzi huo, akiahidi kukomesha kile alichokiita matumizi mabaya ya fedha za umma.



Msimamizi wa uchaguzi Jimbo la Kahama Mjini, Anderson Msumba (kulia), akiwaapisha kiapo cha maadili mawakala wa usimamizi wa uchaguzi 567 kutoka vyama vya siasa jimboni humo, katika Kata ya Nyasubi, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Vilio kila kona viapo mawakala

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimelalamikia kile kinachokiita figisu katika kuapishwa kwa mawakala wa vyama vya siasa watakaosimamia uchaguzi mkuu katika maeneo mbalimbali nchini Jumatano ijayo.

Wakati chama hicho kikidai hayo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeongeza siku tatu kwa ajili ya shughuli hiyo ya kuwalisha viapo mawakala wa vyama vya siasa.

John Manyika, Katibu Mkuu wa CHADEMA, katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, aliitaka NEC kuchukua hatua ili kuhakikisha mawakala wa chama hicho na wa vyama vingine vya upinzani wanaapishwa.

"Katika muda mfupi uliobaki, tume isimamie kuhakikisha kila halmashauri nchini, katika kata mbalimbali nchini mawakala wa CHADEMA wamepewa haki yao ya kuapishwa," alisema.

Mnyika alivitaja baadhi ya vikwazo vilivyoibuka jana katika kuapishwa kwa mawakala kuwa ni mawakala kutokupewa ushahidi wa nakala ya barua ya kuapishwa, hivyo kuwa hatarini kukataliwa kuingia katika vituo vya kupiga kura hapo baadaye kwa kigezo cha kutokutambulika kwenye vituo husika.

Alisema kuwa kwenye baadhi ya maeneo, akitolea mfano Mpwapwa, mawakala wao hawakuapishwa jana kwa maelezo kuwa itapangwa siku nyingine kwa ajili ya shughuli hiyo.

Akifafanua zaidi kuhusu vikwazo hivyo, Mnyika alisema kuwa katika Jimbo la Chato, mawakala wao walikataliwa baada ya Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo kudai saini ya Katibu wa CHADEMA imeghushiwa na hivyo kutokuwatambua mawakala wa chama hicho.

Mnyika alisema kikwazo kingine ni kubadilishwa kwa vituo vya kuapishwa, akidai kuwa hata ajali iliyowapata mawakala wao watano waliofariki dunia jana, ilichagizwa na kubadilishwa ghafla kwa vituo vya viapo.

**SIKU 3 ZAONGEZWA**

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, jana alitangaza tume hiyo kuongeza siku tatu kuanzia jana kwa ajili ya viapo hivyo, akisema uamuzi huo umetokana na kikao cha tume kilichofanyika jana.

"Kwa kuzingatia mamlaka iliyopewa NEC kifungu cha 57 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343 na kifungu cha 58 cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura 292, imeongeza muda wa kuapisha mawakala na vyama vya siasa.

"Tume imefikia uamuzi huo kwa kuzingatia baadhi ya maeneo yana changamoto ya kufikika kwa urahisi kutokana na jiografia hivyo ni vigumu kwa wasimamizi kuwafikia na kuwaapisha kwa mujibu wa sheria," alisema.

Alivitaka vyama kuhakikisha kufuata utaratibu unaokubalika wa kupeleka mawakala kwa sababu kinyume cha hapo hawataapishwa.

Mkoani Arusha, mawakala 11,311 kati ya 11,833 wa Jimbo la Arusha Mjini wameapishwa baada ya kukidhi vigezo huku 522 wakikwashindwa kukidhi vigezo.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo hilo, Dk. John Pima, alitaja baadhi ya vigezo ambavyo wameshindwa kukidhi kuwa ni pamoja na kupigiwa mhuri wa chama zaidi ya mmoja, kutojaza vituo vyao vya kusimamia na kutotiwa saini za makatibu wa vyama vyao.

**●Imeandikwa na Emmanuel Mwamkinga (TUDARCo), Enock Charles, Romana Mallya (DAR), Cynthia Mwilolezi (ARUSHA).**

# JPM aahidi kufufua viwanda vilivyotelekezwa

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais, Dk. John Magufuli (CCM), ameahidi kufufua viwanda vilivyokufa mkoani Kilimanjaro akichaguliwa tena kuendelea kuwa rais wa nchi.

Vilevile, amewaahidi vijana wa Manispaa ya Moshi ajira za kutosha zitakazotokana na kufufuliwa kwa viwanda hivyo, akitolea mfano kuanza kwa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Karanga.

Alitoa ahadi hiyo jana kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika wilayani Moshi wakati akiomba kura kwa wananchi na wanachama wa CCM waliojitokeza kumsikiliza.

Dk. Magufuli alisema katika utekelezaji huo, serikali imeanza kukifufua kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Karanga kinachomilikiwa na Jeshi la Magereza na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Aliwataka wakazi wa Mkoa wa Kilimanjaro kuanza kujipanga kwa kufanya kazi kwa kuwa serikali imeweka mkakati wa kurudisha heshima ya mkoa huo.

Dk. Magufuli pia alisema serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha bei ya umeme inashuka baada ya kukamilika kwa ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Nyerere. Vilevile, alisema amepanga kuliacha taifa likiwa na amani kama walivyofanya watangulizi wake, akiwataka Watanzania kuwapuuza viongozi wanaochochea kufanya maandamano baada ya uchaguzi.

"Mkiona mtu anawahamasisha kuingia barabarani, kuchoma matairi, hana moyo wa Utanzania, ninaomba ndugu zangu mkumbuke kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi, tunahitaji amani, ukiwa na amani nchi inakwenda mbele," alisema.

Dk. Magufuli alikumbusha mafanikio yaliyopatikana mkoani Kilimanjaro kuwa ni pamoja na serikali kujenga jengo la abiria, ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA) na kufufua usafiri wa reli kutoka Dar es Salaam-Tanga-Moshi-Arusha.

Alisema kufufuliwa kwa reli hiyo kumesaidia kushuka kwa gharama za usafirishaji, akitolea mfano usafirishaji wa mbolea ambao umeshuka.

Kwenye sekta ya afya, Dk. Magufuli alisema serikali imenunua vifaa vya kisasa ikiwamo CT-Scan, MRI kwa gharama ya Sh. bilioni 4.5 na kuvipeleka katika Hospitali ya Rufani ya KCMC.

Pia, alisema serikali imefanikisha ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Mawenzi), ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali hiyo kwa gharama ya Sh. bilioni 6.67, ujenzi wa jengo la dharura, kujenga hospitali katika Wilaya za Siha na Rombo na kukarabati Hospitali za Wilaya za Same na Hai.

**MREMA vs JPM**

Awali akiwa Jimbo la Vunjo, Dk. Magufuli alimpongeza Mwenyekiti wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Agustino Mrema, kwa kumpa heshima kwa chama hicho kutosimamisha mgombea wa Rais ili kumuunga mkono. Mrema ambaye anagombea ubunge wa jimbo, aliwasili eneo la Himo kabla ya Dk. Magufuli kufika na alipofika walikumbatiana kisha kupeana zawadi, Mrema akikabidhi mbuzi baada ya kupewa zawadi ya kofia.

"Rais wetu ni nani?... Rais wetu nani?" Mrema alihoji huku wananchi wakiitikia kwa kujibu "Magufuli".

Mrema alitangaza mapema kwamba TLP inamuunga mkono mgombea urais wa CCM kutokana na kazi kubwa aliyoifanya.

Mbali na Mrema, wagombea wengine wa Jimbo la Vunjo ni pamoja na James Mbatia (NCCR-Mageuzi) na Dk. Charles Kimei (CCM).

**●Imeandikwa na Gwamaka Alilipi (MOSHI) na Christina Mwakangale (DAR)**

# Viongozi wa dini watoa msimamo uchaguzi

**Na Gwamaka Alipipi,** MOSHI

VIONGOZI wa dini mkoani Kilimanjaro wamesema hawajakubaliana kuunga mkono chama chochote cha siasa, kwamba wanakemea kauli za kibaguzi zinazotolewa na baadhi ya viongozi wenzao.

Msimamo huo waliutoa jana wakati wa mkutano wa kampeni wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani hapa uliofanyika kwenye Chuo Kikuu cha Ushirika Mashi. Rais John Magufuli, mgombea wa CCM, alihutubia mkutano huo uliojaa maelfu ya watu.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Sheikh wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mlewa Shaban, alisema Kilimanjaro hawapendelei chama chochote na hakuna makubaliano waliyofikia.

Sheikh Shabani alisema: "Sisi viongozi wa dini mkoa wote wa Kilimanjaro tunayo kamati maalum inaitwa kamati ya mahusiano mbalimbali. Katika kamati hiyo, tumefanya mengi tukiwa pamoja. Tumekubaliana kuwa sisi Kilimanjaro hatukipendelei chama chochote na hatujapeana maagizo yoyote.

"Mufti wetu ameshayasema haya mbele yako ukiwa mjini Korogwe. Hatuna haja ya kusema tena, lakini tunasema kwa faida ya Watanzania kwamba wakiona kwenye vyombo vya habari wakielekeza tumchague nani, basi waelewe jambo hilo si kweli," alisema. Kiongozi huyo alisema wanaheshimu serikali iliyoko madarakani na wanatambua kwamba serikali haina dini bali inawajali wananchi wake bila kujali imani, itikadi wala rangi zao.

"Tunafahamu serikali ilivyotutunza, mfano Hospitali (ya Rufani ya Kanda) ya KCMC inavyotuhudumia. Hii hospitali iko chini ya dini fulani, lakini inawahudumia wananchi wote bila kujali imani wala itikadi.

"Kwa kutambua hilo, katika hospitali hiyo inapeleka dawa na kuwalipa madaktari, hivyo hatuwezi kusema kuwa tupo dhidi ya serikali wala kwenda kinyume na serikali kwani tunajua umuhimu wa serikali," alisema.

Naye Mkuu wa Kanisa la Kiinjili ya Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo (pichani), akiwa katika mkutano huo alisema: "Tunamshuru Mungu kwa kukuleta salama Rais Magufuli mkoani Kilimanjaro, tunafuraha kwa kukupokea, shukrani nyingi kwa Mungu.

"Tunamwomba Mungu akulinde kwa kipindi chote utakachokuwa Moshi na safari yako utakapokuwa popote. Sisi wana Kilimanjaro na kwa niaba ya dini zote, tunapenda kufanya maombi kwa nchi yetu, kwako na watu wote. Mungu tuepushe na vurugu za aina zote, tukailinde amani, tuepushe na kutoelewana, majivuno, kiburi na maneno yanayochochea amani."



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Mtaawa Moshi,
Fax: +255 26 2323233
S.L.P 2888,
Baruapepe: ps@mow.go.tz

40470 DODOMA
Tovuti: www.mwtc.go.tz
Tarehe 21-10-2020

**TANGAZO**

• Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 24-10-2020 Kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka TUNDUMA kuelekea **DAR ES SALAAM** gari hilo lenye namba za usajili **T 591 DQU / T 944 DPE**

• Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 21
Upana - mita 3.00
Kimo - mita 4.6

• Njia itakayotumika: TUNDUMA hadi **DAR ES SALAAM** kupitia MBEYA, **MAKAMBAKO, VIGWAZA**

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Mtaawa Moshi,
Fax: +255 26 2323233
S.L.P 2888,
Baruapepe: ps@mow.go.tz
40470 DODOMA
Tovuti: www.mwtc.go.tz
Tarehe 21-10-2020

**TANGAZO**

• Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 24-10-2020 Kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka TUNDUMA kuelekea **DAR ES SALAAM** gari hilo lenye namba za usajili **T 771 DMM / T 410 DDG**

•Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

Urefu - mita 21
Upana - mita 3.00
Kimo -mita 4.6

• Njia itakayotumika: **TUNDUMA** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **MBEYA, MAKAMBAKO, VIGWAZA**

**Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**


**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Maalim Seif atoa masharti kukubali matokeo uchaguzi

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad (pichani), amesema atakubali matokeo ya uchaguzi hata kama atashindwa ikiwa uchaguzi utakuwa huru na wa haki.

Maalim Seif alitoa masharti hayo jana alfajiri wakati akihojiwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kuhusiana na mambo mbalimbali kuelekea uchaguzi mkuu.



Alisema hayo baada ya kuulizwa kama atakubali matokeo yakionyesha ameshindwa kwa mara nyingine.

"Nimewaambia ikiwa uchaguzi utakuwa huru na wa haki, mimi sina tatizo kumpongeza Dk. Hussein Mwinyi (mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi- CCM)," alisema.

Hii ni mara ya sita kwa Maalim Seif kugombea urais wa Zanzibar.

Akizungumzia suala la wagombea wa ACT-Wazalendo ambao wameenguliwa kugombea katika nafasi mbalimbali, alisema chama kilifuata njia za kisheria kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC). Alisema kutokana na hatua hiyo, baadhi walirejeshwa na wengine hawakurejeshwa.

"Tulikata rufaa (rufani) kwa ZEC kwa wale wa Baraza la Uwakilishi wengine wamerejeshwa. Tunakwenda kwenye uchaguzi maeneo mengine ACT- Wazalendo haina wagombea," alisema.

Maalim Seif alisema wagombea wa nafasi ya uwakilishi ambao hawajarejeshwa itakuwa imeshatoka lakini kwa nafasi ya ubunge sheria inaruhusu baada ya uchaguzi wanaweza kufungua kesi mahakamani.

Kuhusu vipaumbele vyake ikiwa atapewa ridhaa ya kuwa rais, alisema kitu cha kwanza atakachokifanya ni kuunganisha wananchi wa Zanzibar ili kuleta maendeleo.

Maalim Seif pia alisema atainua hali ya maisha ya wananchi ambayo hivi sasa wanakabiliwa na hali ya umaskini kiasi kwamba hata mlo kwa siku umekuwa wa taabu.

NMB
Karibu yako

**TANGAZO KWA WADAIWA SUGU WA BENKI YA NMB**

Benki ya NMB inawataarifu wadaiwa sugu wenye mikopo ambayo hawalipi, wanatakiwa kumaliza kulipa madeni yao au kufika katika tawi la NMB lililo karibu kwa ufafanuzi wa jinsi ya kulipa madeni au kukubaliana jinsi ya kulipa madeni yao. Benki inawapa **siku kumi na nne (14)** (Kuanzia Tarehe ya tangazo hili) kutekeleza agizo hili la kulipa deni.

Kukaidi agizo hili, kutachukuliwa kama kuiruhusu benki kuchukua hatua za ziada ikiwamo kutangaza jina lako, ikiambatana na picha au kuchukua hatua zaidi za kisheria ikiwemo kukufungulia kesi ya madai.

Tunawafahamisha kuwa Benki ya NMB haitahusika na athari zozote zitakazotokana na matangazo ya taarifa za wadaiwa sugu watakaokaidi agizo hili.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na tawi la NMB lililo karibu na wewe, au Kitengo cha Maalum cha Ukusanyaji Madeni ndani ya siku 14 zilizotolewa.

**Simu Namba: +255 222 322 038; +255 222 322 395**
**Barua pepe: SAMdepartment@nmbbank.co.tz**

www.nmbbank.co.tz

# Mawakala CHADEMA wafariki katika ajali

**Na Thobias Mwanakatwe**

WATU wanne ambao ni mawakala wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamefariki dunia na wengine wanne kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kupinduka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi (ACP) Justine Masejo, akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka Sumbawanga, alisema tukio hilo lilitokea jana saa 2:30 asubuhi katika kijiji cha Malonje, Sumbawanga Vijijini.

Alisema ajali hiyo imehusisha gari yenye namba za usajili T 381 DZQ aina ya Noah ambalo lilikuwa likiendeshwa na dereva mmoja akiwapeleka mawakala wa CHADEMA katika kijiji cha Sandulula.

Kamanda Masejo alisema gari hilo lilipofika katika kijiji cha Malonje likiwa katika mwendo wa kasi, dereva alishindwa kulimudu wakati wa kukata kona na kupinduka.

Alisema kufuatia tukio hilo, watu watatu walifariki papo hapo na mmoja alipoteza maisha wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Rukwa na miili yao imehifadhiwa kwenye hospitali hiyo.

Aliongeza kuwa majeruhi katika ajali hiyo ni wanne akiwamo dereva wa gari hiyo ambao wote wanaendelea na matibabu katika hospitali hiyo na hali zao zinaendelea vizuri.

Kamanda Masejo alisema majina ya waliofariki pamoja na waliojeruhiwa bado hayajafahamika na Jeshi la Polisi linaendelea kufuatilia kupitia kwa ndugu zao na watajulikana baada ya utambuzi wa ndugu.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa dereva ambaye alishindwa kukata kona na kusababisha gari kupinduka.

Kamanda Masejo alitoa wito kwa madereva kuwa makini wanapoendesha vyombo vya moto kwa kutoendesha kwa mwendo kasi ili kuepusha ajali zisizokuwa za lazima.




Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akizungumza katika kongamano la amani la viongozi wa dini, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuitakia amani nchi kuelekea uchaguzi mkuu ujao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dk. Mwinyi: Najiandaa kushona suti ya ushindi

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ana uhakika wa kushinda nafasi hiyo na kwamba kwa sasa anajiandaa kushona suti ya ushindi.

Akihutubia mkutano wa kampeni jana katika Kijiji cha Kiwani, Wilaya ya Mkoani, Kusini Pemba, Dk. Mwinyi alisema ari ya vijana kuiunga mkono CCM ni dalili kubwa ya kupata ushindi wa kishindo.

Dk. Mwinyi alisema kutokana na vijana wengi ambao ni asilimia kubwa ya wapigakura kumuunga mkono yeye ambaye ni mgombea kijana kuliko wote katika kinyang'anyiro hicho, ana kila sababu ya kushona suti ya ushindi.

"Nataka niwaulize kati ya kijana na mzee mtamchagua nani?" Aliuliza Dk. Mwinyi huku umati uliofika kwenye mkutano huo ukijibu: "Tutamchagua kijana." Mgombea huyo wa urais alisema kwamba zama za sasa ni za vijana, hivyo akishinda Zanzibar atatoa nafasi kubwa kwa vijana.

Dk. Mwinyi, ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 54, anapambana na Maalim Seif Sharif Hamad wa ACT- Wazalendo ambaye ana umri wa miaka 77.

Kuhusu amani, Dk. Mwinyi alisisitiza Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla kulinda na kudunisha amani kwa kuwa ndiyo nguzo muhimu kwa maendeleo. Alisema bila amani hakuna shughuli zozote za maendeleo zinazoweza kufanyika.

Sambamba na amani, aliwataka wana CCM kudumisha Muungano kwa sababu umewaweka karibu na umekuwa na manufaa makubwa kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mkutano huo ulihudhuriwa na umati wa wana CCM katika Jimbo la Kiwani na maeneo mengine ya kisiwani Pemba. Kufikia saa tano asubuhi uwanja ulisheheni wanachama wa CCM na wananchi waliofika kusikiliza ilani, sera na mwelekeo wenye kuleta matumaini kwa wananchi.

**SHEIN AONYA**

Makamu Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, aliyekuwa mgeni rasmi katika mkutano huo, aliwaonya wale wote wanaochezea amani, waache kufanya hivyo, vinginevyo watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

"Wasiwatishe watu, nguvu na uwezo wa kuwadhibiti tunao na tunawaambia tutailinda amani yetu kwa gharama yoyote ile. Wananchi nataka kuwaambia hakuna wa kukutisheni, tembeeni kifua mbele na siku ya uchaguzi nendeni kwa uhuru na mapana kwenda kupiga kura," alisema.

"Tumo katika vuguvugu za kampeni za uchaguzi mkuu. Wasitake kutisha watu na wala hawana uwezo huo. Wasione simba kajikunyata wakadhani paka, nawaambia simba si paka. Wasijaribu," alisisitiza.

Aliwataka wananchi wa Zanzibar kuendelea kuipenda CCM, huku akisema chama hicho kitashinda uchaguzi na kwamba hilo halina mjadala.

"Nasema leo (jana) nikiwa Kiwani, tutawashinda tena ushindi mkubwa. Mwaka huu tutapata ushindi mkubwa sana. Tarehe 28 twendeni tukamchague mgombea wetu Dk. Hussein Mwinyi.

"Dk. Hussein Mwinyi ana uwezo mkubwa wa kujieleza, ana sifa ya kuwa mwadilifu, muungwana, mzalendo wa nchi hii na hana papara. Hana vishindo na huyu ndiyo mwenye sifa za kuongoza Zanzibar. Katika sifa 14 za CCM, anazo yeye ndiyo maana kachaguliwa kuwa mgombea," alisema.

# NEC yapongezwa elimu mpigakura

**Na Beatrice Shayo**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imepongezwa kwa kufanya kazi kubwa ya kutoa elimu ya mpigakura katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya The Right Way (TRW), Wallace Mayunga, alisema NEC imejitahidi kutoa elimu, itakayosaidia kuondoa malalamiko na uchaguzi kuwa wa huru.

Mayunga alisema, bado makundi mbalimbali yanapaswa kuendelea kufikiwa ili kupata elimu hiyo yakiwamo makundi ya wafugaji, wakusanya matunda pamoja na vijana.

"Tumeshuhudia kampeni za sasa zimekuwa za kistaarabu pamoja na kuwa kuna baadhi ya viashiria visivyo vizuri, lakini vyombo vya dola vimekabiliana navyo kwa amani," alisema.

Mayunga aliwaomba waandishi wa habari kuhakikisha wanasaidiana na serikali kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kushiriki uchaguzi usiotokana na rushwa.

Alisema rushwa ya uchaguzi ni tishio kwa chaguzi huru na haki, kwa kuwa rushwa ya aina hiyo inaleta viongozi wasio sahihi na kusababisha kuwapo kwa serikali ya kifisadi.

Mayunga alisema jitihada mbalimbali zinafanywa na serikali kuhakikisha taasisi za umma na vyombo vya dola havitumiki kuchochea matokeo ya uchaguzi.

"Hata chama tawala kimetengwa kabisa na serikali na kwamba hakitumii vibaya nafasi yake kisiasa na vyama vyote vya siasa vinapewa fursa sawa," alisema Mayunga.

Aliwashauri watu wote wenye sifa ya kupiga kura kujitokeza kupiga kura bila kizuizi.

"Vyama vya siasa, wagombea na asasi za kiraia zinapata fursa ya kuufikia umma kwa lengo la kutoa elimu ya uraia bila kuwapo kwa kizuizi cha aina yoyote," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TRW, Justina Shauri, alisema kuwa wao watazamaji wa uchaguzi watahakikisha wanatoa taarifa ya kile walichokiona katika maeneo mbalimbali na si vinginevyo.

Shauri alisema, kuwa wameweka watazamaji katika mikoa 11 nchini ambao wataangalia mwenendo wa uchaguzi na kisha kutoa ripoti ya namna uchaguzi huo ulivyofanyika.

"Sisi tunafuata maelekezo tuliyopewa na NEC hatuwezi kutoka nje ya hiyo, hivyo tutaangalia vyote vinavyojitokeza katika maeneo ya uchaguzi na kisha tutatoa ripoti yetu," alisema.

Aliwataka waangalizi hao kuhakikisha hawapendelei chama kimoja na wasikwende kinyume na majukumu yao.

# Mbaroni madai kukutwa na kadi za kupigia kura

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA



VIONGOZI watano wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika kata ya Gwanumpu, Kakonko mkoani Kigoma wanashikiliwa na Polisi kwa madai ya kukutwa na kadi 14 za kupigia kura kinyume cha sheria za uchaguzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Kamishna Msaidizi (ACP) James Manyama (pichani), alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 10:00 jioni na watu hao walikamatwa wakati jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vikiwa katika operesheni ya kuzuia uhalifu.

Aliwataja wanaoshikiliwa kuwa ni Hezron Vincent, Ezekia Samakere, Sheby Kasuka, Helson Miniho na Lubuye Nchondo.

Kamanda Manyama alisema watuhumiwa hao ambao bado wako rumande kwa mahojiano, walikamatwa wakiwa katika duka la uchapaji na uuzaji nyaraka (stationery) wakidurufu nakala za vitambulisho hivyo.

"Wanadai walichukua kadi ili wapige 'photocopy' nakala za kupeleka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kakonko. Hilo ni kosa kisheria kwa mujibu wa sheria za uchaguzi," alisema.

Kutokana na taarifa hizo, Nipashe ilimtafuta Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Kigoma, Shaban Madege, na kukiri kukamatwa kwa watu hao huku akisema ni mawakala wao.

Madege alisema wanachama hao walikuwa wakiendelea na taratibu za kukamilisha nyaraka kwa ajili ya kuruhusiwa kusimamia uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu.

Alisema mkuu wa wilaya akiongozana na watu wa usalama na msimamizi wa uchaguzi, waliwakuta mawakala hao wakiwa na Katibu wa CHADEMA kata ya Gwanumpu, wakikamilisha taratibu kwa ajili ya kudurufu nyaraka kupeleka ofisi ya msimamizi wa uchaguzi.

Madege alisema eneo hilo halina mashine za kudurufu, hivyo walimpatia kiongozi wao akawatolee.

"Uthibitisho upo kwa msimamizi wa uchaguzi kuwa kadi zilizokamatwa ni za mawakala wetu na barua zingine zilizopaswa waambatanishe zipo na hiki kinachoendelea ni hujuma za uchaguzi," alisema.

# Mvua kubwa yaja mikoa 10

**Na Faustine Feliciane**

MVUA kubwa inatarajiwa kunyesha kwenye mikoa 10 ya Tanzania Bara inayopata mvua mara moja kwa mwaka ambayo ni Mbeya, Iringa, Songwe, Njombe, Morogoro, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Singida na Dodoma.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) jana, ilitoa utabiri wa mwenendo wa mvua kwa maeneo hayo na katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi inatarajiwa kuwa na mvua ya wastani mpaka chini ya wastani.

Akizungumza jana wakati wa kutangaza utabiri huo, Mkurugenzi wa TMA, Dk. Kijazi alisema katika mikoa mingine mvua kubwa inayoweza kuwa mpaka za juu ya wastani inatarajiwa kunyesha na kuzitaka mamlaka kuanza kuchukua tahadhari ya athari zinazoweza kutokea.

"Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa, mvua ya wastani hadi juu ya wastani inatarajiwa katika maeneo mengi ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Kanda ya Kati pamoja na Pwani ya Kusini, hata hivyo mvua nyingi inatarajiwa kunyesha katika wiki ya pili," alisema Dk. Kijazi.

Alisema Kanda ya Magharibi, mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi kunatarajiwa kuwa na mvua kidogo kufikia chini ya wastani, inayotarajia kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi ujao katika mikoa ya Katavi na Tabora na kusambaa Kusini mwa Mkoa wa Kigoma, inayotarajiwa kumalizika wiki ya nne ya mwezi Aprili mwakani.

Kwa Kanda ya Kati, mikoa ya Singida na Dodoma kunatarajiwa kuwa na mvua kubwa na inayotarajiwa kunyesha wiki ya kwanza mpaka ya pili ya mwezi ujao.

"Kwa Nyanda za Juu Kusini Magharibi kwa maana ya mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe na maeneo ya Kusini mwa Mkoa wa Morogoro, kutakuwa na mvua kubwa hadi kufikia juu ya wastani ukiondoa Mkoa wa Rukwa ambako kutakuwa na mvua chache kufikia chini ya wastani, mvua hiyo itaanza wiki ya pili ya mwezi Novemba," alisema.

Pia mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kunatarajiwa kuwa na mvua kubwa mpaka kufikia juu ya wastani na itaanza kunyesha wiki ya pili ya mwezi ujao na kumalizia wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili, mwakani.

"Ni vyema sasa mamlaka husika na wananchi kwa ujumla katika maeneo niliyoyataja kuanza kuchukua tahadhari kukabiliana na athari zitakazojitokeza katika maeneo yao."


BIASHARA ZOTE MAKINI
HUTANGAZWA HAPA
Nipashe | Nipashe mwendo mdundo
Unafahamu ni kwa nini?
"Tunaongoza na Kuaminika"




Nipashe MWANGA WA JAMII
WASILIANA NASI
0745 700 710 au 0677 020 701
advertise@guardian.co.tz (Matangazo)
subscription@guardian.co.tz (Magazeti)
epaper@guardian.co.tz (epaper)
PATA NAKALA YAKO
https://epaper.ippmedia.com
Pakua The Guardian-IPP Media
App Store | Google Play
KUWA WA KWANZA KUHABARIKA
TUFUATE nipashetz | nipashe | TheGuardiantz | YouTube TheGuardiantz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera TAKUKURU kuokoa fedha za wastaafu

**MARA** kwa mara Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewasaidia wastaafu kuokoa fedha zao, ambazo walitapeliwa na watu kwa namna tofauti.

Mathalani tukio la juzi, TAKUKURU mkoani Singida iliokoa zaidi ya Sh. milioni 46 za pensheni ya walimu waliokuwa wamedhulumiwa na mkopeshaji haramu ambaye alikuwa anatoa mikopo umiza.

Baada ya dhoruba hiyo walimu hao walitoa taarifa TAKUKURU kwamba baada ya kustaafu walikuwa wanakopa fedha kidogo kidogo kutoka kwa mkopeshaji na kufikisha jumla ya shilingi milioni tisa kwa mwalimu mmoja na shilingi milioni mbili kwa mwalimu mwingine.Walimu hao walipewa mikopo hiyo kwa makubaliano ya kulipa kupitia fedha za pensheni watakazolipwa baadaye.

Baada ya walimu hao kupokea pensheni zao, mkopeshaji huyo aliwaongozea kiasi kikubwa cha riba tofauti na walivyokubaliana na walidaiwa kulipa Sh. milioni 22.5 kutokana na mkopo ambayo ni sawa na riba ya asilimia 215 kwa mwalimu wa kwanza na Sh. milioni 24 ambayo ni sawa na asilimia 120.

Aina hii ya mikopo inatolewa sana mitaani na wengi wananaswa kutokana na shida zinazowakabili na kujikuta wanazama kwenye mikopo hiyo ambayo inawagharimu kiasi cha wengine mali zao kupigwa mnada ili kulipa madeni.

Jana kuna taarifa zilizoripotiwa kuwa watoto wawili wamemchoma mama yao ambaye aliweka rehani nyumba mbili za baba yao na kupewa mkopo ambao alishindwa kulipa.

Wote hawa walikopa kutokana na shida zilizokuwa zinawakabili kwa wakati huo kiasi cha kushindwa kuangalia riba zitakuwa za aina gani na watawezaje kulipa kwa wakati.

Kazi inayofanywa na TAKUKURU ni nzuri kwa kuwa inahakikisha wananchi wanapata haki zao dhidi ya waliowaumiza kama ilivyojitokeza kwa walimu hao. Lakini inatoa fundisho kwa kila Mtanzania kujifunza kujipanga kimaisha hasa maisha kabla ya kustaafu kuwa na akiba itakayomwezesha kuendelea na maisha hadi pensheni yake itakapotoka. Kundi la wananchi wanaoathiriwa zaidi na mikopo umiza ni walimu ambao baadhi yao wakati wakiwa kazini wanakopa fedha bila kuangalia riba husika na madhara yake.

Wapo ambao wanakopesha na kubaki na kadi ya benki na kila mshahara wa mwalimu husika unapoingia aliyemkopesha anakwenda kuchukua fedha hadi mkopo utakapoisha.

Wakati mwingine walimu bila kujua na kutaka kupata fedha kutatua changamoto zao wamejikuta wakiishi kwa madeni makubwa, ikiwamo mikopo kiasi cha mshahara wake wote kwisha.

Mwalimu huyo huyo amekopa benki, amekopa kwenye taasisi ya fedha na amekopa kwa watu binafsi, na bado ana makato ya kisheria ya kodi, hifadhi ya jamii, bima ya afya, chama cha walimu na mkopo wa elimu ya juu.

Kwa hali hii mwalimu huyu hawezi kuwa na amani bali muda mwingi atakuwa anahangaika kuishi maisha ya kulipa madeni, na anapostaafu kwa kuwa huona atapata fedha nyingi basi huingia makubaliano ambayo yanamuumiza.


Lakini pia jambo hili linatoa elimu kwa mifuko ya hifadhi ya jamii kuwajibika kwa wanachama wao kwa kuwapa mafao yao kwa wakati, kwa kuwa bado kuna malalamiko ya kucheleweshewa mafao ya mkupuo na ya mwezi baada ya kustaafu, kiasi cha wengi kuingia matamanio ya kukopa kwa kuwa kuna ahadi za kupata fedha hizo karibuni. Imekuwa kawaida wastaafu kupewa ahadi ya fedha zao kuingia benki siku fulani na wakati mwingine zinachelewa na kuwa chanzo cha wastaafu kukopa kwa matarajio ya kulipa ili kutatua changamoto zinazowakabili.

Ni muhimu sana kila mmoja kuwajibika ili kuondokana na hali hizi ambazo kwa namna moja au nyingine zinachangia walimu kuingia kwenye mitego ya wakopaji ambao huwapa mikopo umiza.


Kwa mamlaka nyingine za serikali ziendelee kuwachukulia hatua wakopeshaji hao na kusaidia jamii kuondokana na maumivu hayo ikiwa ni pamoja na jamii kutoa taarifa za matukio kama haya sehemu husika kama TAKUKURU.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Tusikilize sera na tufanye uamuzi sahihi, Oktoba 28

**AHADI** 'nitafanya nini' na kunadi sera ndiyo bidhaa kuu zinazonadiwa kwenye kampeni za uchaguzi kama kinachojiri sasa.

Leo hii zimesalia siku sita pekee, kutimu watu ya kupanga foleni nchi nzima, kila moja mahali pake alikojisajili na kazi ni moja tu; kudumbukiza kura yake alikopangiwa.

Dakika za lala salama ni mambo yatakayosikilizwa sana ndani ya kampeni zinazoendelea. Pengine ni vyema sasa kampeni zinazoendelea nchini, kuwachagua madiwani, wabunge na Rais.

Katika hilo, sera zimekuwa zikitolewa katika mikutano yao mbalimbali kuwaomba wananchi wawachague hicho wanachokinadi, kila mgombea anatoa sera kuonyesha kipindi cha miaka mitano, kile atakachokifanyia taifa.

Katika kampeni hizo kuelekea uchaguzi, vyama vyote vinanadi sera, ambazo kimsingi wananadi kile watachokifanyia taifa, picha zao zimetapakaa mitaani kote mijini na vijijini.

Ni mahali kunashuhudiwa sera zilizowekwa kile watakachokifanyia taifa waingiapo madarakani.

Kuwekwa kwa sera katika picha, ni moja ya njia kumuwezesha msomaji bango, ajue kile anachoenda kukipigia kura Oktoba 28 au Jumatano ijayo, awe ameamua kwa usahihi.

Hivyo ni jukumu letu wote tuliofikisha umri wa kupiga kura, kupitia vitambulisho vyetu, kuendelea kuwasikiliza wagombea na mwisho kufanya uamuzi sahihi.

Makundi mengi ya watu wa rika mbalimbali, wamekuwa wakijitokeza kusikiliza sera za wagombeaji, katika kipindi kiliochopo cha majeruhi katika kampeni.

Hapo niseme, kama makundi hayo yanayojitokeza kusikiliza sera, wakiwa tayari wameshajiandikisha katika katika daftari la kupiga kura, wanatakiwa Oktoba 28 wafike kupioga kura wakiwa na uamuzi sahihi kwa

> **Hapo niseme, kama makundi hayo yanayojitokeza kusikiliza sera, wakiwa tayari wameshajiandikisha katika katika daftari la kupiga kura, wanatakiwa Oktoba 28 wafike kupioga kura wakiwa na uamuzi sahihi kwa anayemuona sera yake, inaweza kuchangia mabadiliko makubwa kimaendeleo, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.**

anayemuona sera yake, inaweza kuchangia mabadiliko makubwa kimaendeleo, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Niseme, ni jambo linalosikitisha pale watu waliokuwa na umri wa kupiga kura, wanashindwa kupiga kura kwa sababu zisizo na mashiko. Vitambulisho vimekuwa vikitolewa kwa wapiga kura, lengo kuu ni kuwezesha kutumia haki yako ya kikatiba kwa kupiga kura.

Kuna ushuhuda wa yasiyo na mashiko, kuwapo watu ambao wana vitambulisho, lakini panapofanyika uchaguzi, hawajitokezi kupiga kufanya hivyo.

Kinachotakiwa hapo ni kwamba, mtu atimize haki yake ya kikatiba kwa kutimiza malengo, akipiga kura katika namna sahihi.

Mtu anashindwa kutimiza lengo husika, huku akiwa na kitambulisho sahihi cha kupiga kura, alipojisajili kwa hiari yake. Hapo niseme, hatua inachukuliwa kwa kutimiza haki husika ya kikatiba, ambayo inatambua umri na sifa zinginezo za upigaji kura.

Vitambulisho hivyo pamoja na kutumiwa katika nafsi ya utambulisho binafsi wa mtu anapotakiwa kukionyesha, basi Oktoba 28 kinapaswa kutumika kupigia kura.

Ni mazingira yanayomsaidia mtu kumpata kiongozi atakayeleta maendeleo katika eneo lake na ndio maana kunazaliwa tafsiri au ufafanuzi kwamba, 'itafungua njia ya maendeleo.'

Hivyo, ni mustakabali wa kuzaliwa tafsiri kuwa mtaka maendeleo akishindwa kupiga kura, atakuwa amejikosesha fursaya maendeleo stahiki.

Mara nyingi inaelezwa maendeleo yanaletwa kwa nguvu ya pamoja, pale jamii inapokubaliana kujiunga kuwa kitu kimoja na kutumia haki za kikatiba kupiga kura .

# Bosi mpya WFP awasilisha hati kwa serikali

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKILISHI mpya wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon-Gibson, amewasilisha hati za utambulisho kwa serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, zilizopokelewa na waziri wa wizara hiyo, Profesa Palamagamba Kabudi.

"Nina furaha kubwa kurudi Tanzania na kuona kwamba nchi imepiga hatua kubwa katika viashiria muhimu vya maendeleo ya watu na ya kiuchumi," alisema Gordon-Gibson na kuongeza: "Tunaendelea kudhamiria kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kukabiliana na changamoto zake za kitaifa hususan kuhusu mazingira, tabia ya nchi, skimu za kinga ya jamii, uzalishaji katika kilimo na mifumo ya chakula, mlo kamili na lishe bora, na pia usawa na uwezeshaji wanawake."

Taarifa iliyotolewa na WFP kwa vyombo vya habari jana, ilisema Gordon-Gibson, ambaye ni mwanasheria kwa taaluma, amefanya kazi na WFP kwa zaidi ya miaka 20. Katika miaka miwili iliyopita, alifanya kazi kama Mwakilishi wa WFP nchini Jordan, ambayo ni miongoni mwa operesheni kubwa za shirika hilo duniani.

Pia, alitumikia kama Mwakilishi wa nchi Jamhuri ya Kidemokrasi ya Watu wa Lao kwa miaka mitatu. Kazi yake ya miaka ya hivi karibuni zaidi ilikuwa ni Naibu Mwakilishi wa nchi za Tanzania, Myanmar na Niger.

Katika kuisaidia Tanzania kufikia nchi yenye uchumi wa kati, WFP inajishughulisha katika maeneo ya lishe, mtandao wa usalama wa kijamii, ugavi wa chakula na kuwasaidia wakulima wadogo. Pia, inawasaidia wakulima hao kupanda ngazi kutoka kufanya kilimo cha kujikimu kwenda cha kibiashara na kupata masoko ya uhakika kwa lengo la kuzifanya jamii za wakulima kuwa na usalama wa chakula zaidi, kujitegemea na kuhimili majanga.


Shirika hilo pia linatoa msaada wa chakula kwa wakimbizi na inatafuta njia za kiubunifu za kuleta maendeleo endelevu.

Taarifa hiyo ilisema, WFP pia inafanya kazi za kilojistiki kwa ajili ya nchi zisizopakana na bahari zilizo jirani na Tanzania na ina mchango muhimu katika ukanda wa Afrika Mashariki katika kuwezesha usafirishaji wa chakula ili kuokoa uhai wa watu walio katika migogoro. "Inashirikiana kwa karibu na Serikali ya Tanzania ili kuimarisha nafasi ya nchi kama lango kuu la bahari na mtoaji mkubwa wa chakula katika ukanda huu," ilisema taarifa hiyo.

Gordon-Gibson alisema WFP ina thamini ushirika wake na Serikali ya Tanzania: "Sehemu muhimu ya ahadi yetu ni kuisaidia serikali kukabiliana na mahitaji ya wale walio na shida zaidi na wasio na usalama wa chakula nchini Tanzania kwa kuleta pamoja utaalamu, uwezo na rasilimali zetu na kushirikiana zaidi kuliko hapo kabla ili kumaliza njaa na utapiamlo hadi ifikapo mwaka 2030."

Shirika la Mpango wa Chakula Duniani ni mshindi wa tuzo ya amani ya Nobel ya 2020.

"Ndiyo shirika kubwa zaidi la kibinadamu, tunaokoa maisha katika dharura na tunatoa msaada wa chakula kujenga amani, utulivu na ustawi kwa watu walioathirika na mizozo, maafa na athari za mabadiliko ya tabia nchi."



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akipokea nakala ya hati za utambulisho ya Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon-Gibson, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# 'Watanzania wana mwamko kutumia wataalamu ukaguzi'

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Kampuni ya Kimataifa ya Ukaguzi wa Hesabu Mazars, Witnes Shilekwirwa, amesema Watanzania wana mwamko mkubwa wa kutumia wataalamu wa ukaguzi wa mahesabu kukwepa faini za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema hayo wakati wa utambulisho wa chapa inayotambulisha uwapo wao ndani na nje ya nchi na kupata kazi nyingi ambazo zitasaidia kuongeza mapato ya kodi nchini.

"Watanzania wamekuwa na mwamko mkubwa wa kutumia wataalamu wa ukaguzi kwa sababu wanapoteza pesa nyingi za kulipa faini kwa kutofuata sheria," alisema Shilekwira.

"Sasa hivi TRA mifumo yao imekuwa kwenye 'online' inalazimisha kuwa na wakaguzi na sheria ya nchi inataka kila mtu mwenye mapato yanayozidi shilingi milioni mia moja awe na mtu wa kumkagua." Alisema kampuni hiyo imepanua wigo katika nchi zaidi ya 90 ili kuleta mafanikio na mtazamo tofauti katika kazi ya ukaguzi huduma za kodi na ushauri.

Shilekirwa alisema mabadiliko ya chapa yao yanathibitisha mkakati wa kujenga ulimwengu wa haki na mafanikio.

Pia, wanajivunia chapa mpya inayotambulisha na kuwaweka kwenye mtazamo tofauti kitaifa na kimataifa na kuendana na mabadiliko. Mkurugenzi Mtendaji wa Mazars Group, Herve Helias, katika ujumbe wake alisema anafurahia uzinduzi wa kitambulisho kipya baada ya miaka miwili ya ushauri na washirika wake.

Aliongeza kuwa katika kila nchi ambayo Mazars inafanyia kazi washirika wake huchanganya uelewa wa kitamaduni wa nchi husika na mtazamo wa kimataifa ikihudumia wateja wa aina mbalimbali kwa ushirikiano wa kweli ambao unawapa ujasiri katika biashara zao na kuwasaidia kufanikisha azma zao.

Alisema Mazars inawekeza kwenye idara ya ukaguzi kwa kufundisha na kutoa wataalamu kuwekeza kwenye teknolojia na udhibiti wa ubora idara ambayo inahitaji kuwekeza kwenye utaalamu na ubunifu.

# Tigo, ITEL zazindua simu mpya Itel T20

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo, imeungana na ITEL kuzindua simu janja mpya ya ITEL T20 jijini Dar es Salaam.

Kampuni hiyo inayoongoza kwa kutoa huduma za mawasiliano ya kidigitali, ilizindua simu hiyo katika hafla iliyofanyika jana.

Mkumbo Myonga, Mkuu wa Kitengo cha Vifaa vya Mawasiliano wa Tigo Tanzania, alisema: "Ushirikiano wetu na Transsion Holdings tunaubeba kwa fahari kubwa kwa sababu unaenda sambamba na dira yetu ya kuhakikisha tunatoa huduma bora za kisasa kwa wateja wetu wote.

"Uzinduzi huu wa leo (jana) ni wa simu nyingine ya kisasa kabisa na ya gharama nafuu ni uthibitisho kwamba tumejizatiti kuhakikisha kila mteja wetu anafurahia matunda ya vifaa hivi vipya vya kisasa ambavyo vimeunganishwa na huduma bora za kidigitali zinazotolewa na Tigo."

Alisema wapo kwa ajili ya kuendelea kutimiza ahadi zao kwa Watanzania za kuhakikisha kila raia anafurahia kutumia simu janja za kisasa huku akiwa ameunganishwa na mtandao wa 4G ulioenea kote nchini.

Myonga alisema simu hizo mpya zinapatikana katika maduka yote nchi nzima na pia ITEL T20 inakuja ikiwa na ofa ya GB 30 za intaneti ambazo zitatumika kwa mwaka mzima.

"ITEL T20 ni simu mpya yenye huduma za kisasa za simu janja zenye uwezo wa 4G na itakuwa inapatikana kwa kiasi cha shilingi 84,900 tu", alisema Myonga.

Naye Ofisa Uhusiano wa ITEL, Fernando Wolle, alisema amefurahishwa na ubia huo na Tigo Tanzania katika uzinduzi wa simu janja ya ITEL T20.

"Tumeingia ubia huu na Tigo ili kuongeza thamani ya simu yetu. ITEL T20 ni zaidi ya simu janja nyingine kwa sababu imewekwa huduma nyingi za kidigitali. ITEL T20 ni simu janja yenye uwezo wa 4G ikiwa na ukubwa wa screen wa nchi tano na uwezo wa 1GB+16GB, huku ikiwa inafanya kazi kwa kutumia mfumo mpya wa Android P Go edition OS. Jina T20 linawakilisha, T= Tigon a 20 inawakilisha mwaka 202," alisema Wolle.

# Nyumbu kutengeneza magari ya zimamoto

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania (CGF), John Masunga, amesema jeshi hilo limeingia mkataba na Shirika la Nyumbu linalomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kwa ajili ya kutengeneza magari ya kuzima moto kukabiliana na majanga ya moto yanayotokea kwenye mabweni ya shule nchini.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa alipokuwa katika ziara ya ukaguzi wa ofisi zake pamoja na vitendea kazi.

Masunga alisema, akiwa mkoani humo ameona kuna tatizo la uhaba wa magari na katika kukabiliana nalo, jeshi limeingia mkataba wa Shirika la Nyumbu kwa ajili ya kutengeneza magari ya kuzima moto.

"Ninaweza kusema tumeshaanza hatua ya awali, tumeanza na magari sita na yanachukua muda mrefu kidogo kuanzia miezi 12 hadi 15 kuwa tayari na mkataba huu utakuwa endelevu kila mwaka," alisisitiza Kamishna Jenerali Masunga.

Hata hivyo, alisema magari mengine ya kuzima moto yataendelea kununuliwa kutokana na fedha zinazotengwa na serikali kwenye bajeti yake.

Kuhusu majanga ya moto katika shule mbalimbali nchini, alisema tayari kimeundwa kikosi kazi ambacho kinafuatilia matukio hayo na muda si mrefu taarifa itakuwa wazi ili Watanzania wajue hali ikoje kwenye matukio hayo.

"Juhudi pia zinaendelea kwenye vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha matukio haya yanakoma kabisa kwa hiyo tuwe na subira kuhusiana na tamko la hayo majanga ya moto shuleni," alisema Masunga.

Aliwataka wamiliki wa shule wote wahakikishe shule zao zinakaguliwa na jeshi hilo na kufanyiwa ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto. Kuhusu ajali za moto kwa magari ya kubeba mafuta, alisema matukio hayo yapo katika barabara kuu zinazopita mkoani Morogoro na tayari amefanya mazungumzo na Katibu Tawala wa mkoa huo, Mhandisi Emmanuel Kalobelo na moja ya makubaliano ni kuongeza magari ya kuzima moto pamoja na utoaji wa elimu ya kuzuia majanga ya moto.

Pamoja na hayo, alisema jeshi hilo linaendelea kushirikiana na mamlaka zingine hasa za halmashauri za miji, Manispaa na majiji kuwa wanapoweka mipango miji kuweka miundombinu rafiki ya kukabiliana na majanga ya moto na miradi ya maji inapojengwa waweke pia visima vya maji kwa ajili ya matumizi ya jeshi hilo.

Akizungumzia suala hilo, mmoja wa wakazi wa Manispaa ya Morogoro, Bernald Lienda, aliishauri serikali umuhimu wa kuingiza kwenye mitaala ya elimu suala ya uzimaji moto ili wanafunzi waweze kuwa tayari majanga hayo yanapotokea.

Alisema licha ya shule hizo kwa sasa kutokuwa na vifaa vya kuzimia moto, hata vikiwekwa wanafunzi watashindwa kuvitumia kutokana na kukosa elimu.




Mkuu wa Kitengo cha Vifaa vya Mawasiliano kutoka Tigo Tanzania, Mkumbo Myonga (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa simu janja mpya za ITEL T20. Kulia ni Ofisa Uhusiano wa ITEL, Fernando Wolle. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Agricom kumsaidia mkulima zana bora

**Na Beatrice Shayo**

WAKULIMA wameshauriwa kutumia mfumo wa kisasa wenye zana bora ambazo zitawawezesha kuwa na kilimo chenye tija.

Kaimu Meneja Mkuu na Mkuu wa Idara ya Mauzo na Masoko wa Agricom Africa Limited, Remmy Nindi, alisema hayo akiwasilisha mada katika kikao cha warajisi wasaidizi wa mikoa 26 chini ya Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika (TCDC).

Alisema kumekuwa na upatikanaji wa mazao chini ya viwango kwa sababu ya wakulima kuendelea kutumia mfumo wa kizamani na kusababisha kushindwa kukua kiuchumi. "Mfano mzuri kwenye mahindi upigaji wa mahindi bado ni tatizo mwisho wa siku yanayopatikana yapo chini ya kiwango," alisema.

Pia, alisema kwenye zao la dengu wanatumia trekta kwa ajili ya kupiga jambo ambalo ni hatari kwa afya.

Nindi alisema wakitumia zana bora ambazo wanazitoa zitawasaidia kuwaongezea tija, kupunguza muda na kupata kiwango bora cha mazao.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuwafahamisha warajisi matumizi sahihi ya zana za kilimo zinazouzwa na kampuni ya Agricom ili wakawe mabalozi kwenye vyama vya ushirika.

Alisema ni muhimu kuwaelimisha wakulima umuhimu wa kununua zana bora, wanapojiandaa na misimu yote ya kilimo kuanzia maandalizi ya shamba na baada ya mavuno.

Nindi alisema Agricom inatoa huduma za upatikanaji wa vipuli, matengenezo, kuunganisha na taasisi za fedha zinazotoa mikopo ya zana za kilimo, uuzaji wa vifaa (matrekta na majembe, vifaa vya mafunzo na maeneo ya maonyesho).

"Agricom inajihusisha na uuzaji wa zana bora za kilimo kwa ajili ya maandalizi ya shamba kama vile matrekta, mashine ya kuchabanga, kutifua udongo, mashine za kupanda mbegu, mashine ya kupuliza dawa, mashine ya kusambaza mbolea shambani na mashine za kuchimba mashimbo," alisema Nindi.

Alisema mkakati wao ni kumsaidia mkulima kuwa na kilimo chenye tija ambacho atakifurahia kwa kuongeza uchumi wake na kuachana na kilimo cha zamani.

# Ujenzi wa barabara waleta neema Simiyu

**Na Happy Severine,** BARIADI

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Issac Kamwelwe, amesema kukamilika kwa barabara ya Bariadi hadi Maswa yenye urefu wa kilometa 49 kwa kiwango cha lami, kumesaidia kurahisisha shughuli za kibiashara mkoani hapa.

Kamwelwe alisema hayo jana wakati akikagua barabara hiyo eneo la Kidulya mjini hapa na kueleza ameridhishwa na mkandarasi kutokana na kasi aliyoitumia kukamilisha kazi hiyo.

Alisema Mkoa wa Simiyu ambao hapo awali wananchi wake walikuwa wakipata adha ya usafi na kuendesha shughuli zao za kibiashara ipasavyo, kwa sasa wanafanya biashara na kusafiri bila matatizo.

Waziri aliwashukuru Watanzania wote walipakodi kwa kuwa kodi zao zinatumika vizuri katika kuleta maendeleo ya wananchi wote na kusihi waendelee kuwa walipaji kodi wazuri.

"Nawashukuru sana Watanzania walipa kodi wazuri kwani wao wamesaidia sana kuleta maendeleo ya nchi hususani katika sekta yangu. Miradi mingi ya usafirishaji na uchukuzi imekamilika kwa viwango vinavyotakiwa," alisema.

Kamwelwe pia alisema kwa sasa kuna barabara kadhaa zinazounganisha mkoa wa Simiyu na wa Singida bado hayafikiki vizuri, lakini tayari usanifu wa barabara ya Bariadi –Itilima, Mwandoya- Sibiti, Mkalama na Iguguno wameanza kufanyiwa usanifu na siku si nyingi ujenzi utaanza ili kuruhusu barabara hizo zipitike bila shida.



Mafundi wa kampuni ya Nipo, wakishusha vifaa vya ujenzi wa barabara katika eneo la Makumbusho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ujenzi reli Mtwara-Mbamba Bay waiva

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amesema serikali inatarajia kuanza ujenzi wa reli ya kimataifa ya kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay ikiwa na matawi Mchuchuma na Liganga, Ludewa mkoani Njombe.

Majaliwa alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wakazi wa Ndanda, wilayani Masasi katika mkutano wa kampeni za CCM uliofanyika kwenye uwanja wa mpira wa Njenga.

Majaliwa ambaye ni Waziri Mkuu wa Tanzania yuko mkoani Mtwara kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli.

Alitumia fursa hiyo kumnadi mgombea ubunge wa Jimbo la Ndanda, Cecil Mwambe na mgombea udiwani wa kata ya Njenga, Ester-Stella Kambanga na wagombea udiwani wengine wa CCM.

"Upembuzi yakinifu tayari umeshafanyika na michoro yote iko tayari. Na hii iko kwenye ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, ibara ya 59 (d)," alisema.

Ibara ya 59 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasema: "Katika miaka mitano ijayo, chama kitaielekeza serikali iendelee kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati. Miundombinu hiyo inajumuisha ya reli, viwanja vya ndege na bandari. Pia kuboresha huduma za usafiri wa anga, baharini na kwenye maziwa kwa kununua vyombo vipya vya usafiri na kukarabati vilivyopo ili kuimarisha huduma."

Kifungu (d) cha ilani hiyo kinabainisha kwamba ili kufikia azma hiyo, katika kipindi hicho, miradi itakayotekelezwa katika maeneo mbalimbali ni pamoja na ujenzi wa reli ya Mtwara - Songea - Mbamba Bay na matawi ya Liganga na Mchuchuma yenye urefu wa kilomita 1,000.

Kuhusu maji, Majaliwa alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 11.2 kwa ajili ya miradi ya maji ya Shaurimoyo, Mkalola, Mpitimbi, Shitingi, Sindano na Lihecha.

Akizungumzia uboreshaji wa barabara, Majaliwa alisema ujenzi wa barabara ya Nanganga - Ruangwa kwa kiwango cha lami, mkandarasi ameshafika kwenye eneo la kazi na ameshaanza kutekeleza ujenzi huo.

Alizitaja barabara zingine ambazo ziko mbioni kujengwa kuwa ni Masasi - Nachingwea (kilomita 45), Nachingwea - Ruangwa (kilomita 50) na Nanganga - Masasi yenye urefu wa kilomita 45.

Majaliwa alisema Shule ya Sekondari ya Ndanda ni miongoni mwa shule kongwe zinazotupiwa jicho na serikali na tayari Sh. milioni 600 zilishatolewa ili kuanza ukarabati wa bwalo.

"Tunataka hii shule irudie kwenye hadhi yake ya zamani," alisema huku akiwataka wanafunzi wa Ndanda wasome kwa bidii ili watimize ndoto zao na serikali itaendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu.

"Wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita wana fursa ya kupata mikopo ya kuendelea na elimu ya juu kwani serikali hii imeongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu kutoka Sh. bilioni 348.7 na sasa hivi tunatoa Sh. bilioni 464," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Majaliwa, wanafunzi wa elimu ya juu wanaopata mikopo wamefikia 130,883 kutoka 98,300 na pia ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini hivi sasa ni 87,813 kutoka 65,064 wa mwaka 2015.

# Vijana waonywa kuhusu vurugu

**Na Neema Hussein,** KATAVI

VIONGOZI wa dini mkoani Katavi, wamewataka vijana kutotumika kuvuruga amani ya nchi kwa kufanya vurugu baada ya kumaliza kupiga kura.

Sheikh wa Mkoa wa Katavi, Mashaka Kakulukulu, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya Mkoa, alisema juzi kuwa uchaguzi ni wa muda mfupi, hivyo Watanzania wataendelea na maisha mengine baada ya hapo. Alisema hayo alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema wanaishukuru Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuweka miundombinu rafiki hasa pale waliporuhusu vitambulisho vingine vitumike kupigia kura kwa wale ambao hawana kitambulisho cha kupigia kura.

Sheikh Kakulukuli alisema viongozi wa dini wanaamini kwamba uchaguzi utakuwa huru na wa haki, hivyo kila mtu ajitokeze kutimiza haki yake ya msingi itakapofika siku hiyo.

Alisema mtu anayemaliza kupiga kura ni vizuri akarudi nyumbani kusubiri matokeo yatangazwe pamoja na kuendelea na majukumu yake kuliko kusubiri akiwa katika kituo cha kupigia kura.

Katibu wa Kamati hiyo, George Kisapa, alisema wanazidi kusisitiza haki itendeke kwa kila mgombea aliyeshinda kupewa haki yake badala ya kufanya udanganyifu ambao unaweza kusababisha migogoro na uvunjifu wa amani.

# Neema yanukia Songea ujio Bombardier

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 37 kwa ajili ya ukarabati wa uwanja wa ndege wa Songea ambao utawezesha kwa wakati mmoja kubeba ndege sita aina ya Bombardier.

Akitoa taarifa ya ukarabati wa kiwanja hicho juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Songea, Jordan Mchami, alisema kazi ya ujenzi wa barabara ya kutua ndege yenye urefu wa mita 1,740 na upana wa mita 30 imeshakamilika. Alisema ujenzi wa maegesho ya ndege yenye ukubwa wa mita 139 kwa 126 unatarajiwa kukamilika katikati ya mwezi ujao, hivyo kumudu kuegesha ndege kubwa sita kwa wakati mmoja.

Meneja huyo alisema pia yamejengwa maegesho maalum ya ndege za dharura yenye ukubwa wa mita 70 kwa 40 na kwamba katika kiwanja hicho, zimejengwa taa za kisasa za kuongozea ndege wakati wa usiku, hivyo kuwezesha ndege kutua saa 24.

"Ndege aina ya Bombardier sasa zitaanza kutua wakati wowote katika kiwanja cha ndege cha Songea. Tunatarajia ndege ya kwanza itatua kabla ya mwisho wa mwezi huu," alisema Mchami.

Alisema jengo jipya la abiria lenye uwezo wa kuchukua watu 150 kwa wakati mmoja, limejengwa na kukamilika hali ambayo inaweza kumudu abiria wa ndege mbili za Bombardier kwa wakati mmoja.

Mchami pia alisema gharama za nauli katika ndege hizo za serikali zitakuwa chini kulinganisha na ndege ndogo za kampuni binafsi ambazo nauli yake ni kati ya Sh. 500,000 na 600,000 hali ambayo wananchi wengi hawawezi kumudu.

Kwa mujibu wa Mchami, ujio wa ndege za Bombardier utakuwa ukombozi kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa sababu nauli ya kwenda na kurudi Dar es Salaam na Songea itakuwa Sh. 400,000 tu.

Akizungumza baada ya kukagua ukarabati wa uwanja huo, Mndeme alipongeza kampuni ya CHICCO inayofanya kazi hiyo ambayo itakamilika kwa asilimia 100 ifikapo Desemba, mwaka huu.

Mndeme alisema Uwanja wa Ndege wa Songea ni rasilimali adimu inayoweza kusaidia kukuza uchumi wa mkoa hasa kupitia sekta ya utalii, baada ya kuanzishwa mpango mkakati wa kukuza utalii katika mkoa.

Songea ni miongoni mwa viwanja bora vya ndege Tanzania ambacho kilijengwa kati ya mwaka 1974 na 1980 na kiliwekewa lami, hivyo kuwa na uwezo wa kutua ndege majira yote ya mwaka.

## Walia na utitiri tozo pembejeo

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAUZAJI wadogo wa pembejeo mkoani Kigoma wameiomba serikali iwasaidie kuondoa utitiri wa tozo katika biashara hiyo, ili kuwawezesha kunufaika na utoaji wa huduma hiyo.

Ombi hilo walilitoa juzi wakati wa kikao cha tathmini ya kuhitimisha mradi wa Tija Tanzania uliotekelezwa kuanzia mwaka 2017 hadi nmwaka huu chini ya asasi isiyo ya kiserikali ya kilimo biashara (RUCODIA).

Mmoja wa wauzaji hao, Evelyne William, alisema vigezo vya kuuza viuatilifu wanahitajika kupata cheti kwa Sh. 320,000 na Sh. 200,000 za uzinduzi wa cheti na Sh. 50,000 za kuzindua cheti kila mwaka.

"Mara uzindue cheti, mara ulipie cheti, cheti umeshasomea umepata bado unalipia kibali Sh. 200,000 huku bado kila mwaka unalipoa Sh. 50,000 na bado umeshalipia TRA (Mamlaka ya Mapato," alisema.

Naye Hussen Midyano, mkulima kutoka Wilaya ya Kibondo, alisema wakulima wanakabiliwa na hali duni ya kiuchumi, hivyo kushindwa kumudu mahitaji ya uendeshaji ikiwamo ununuzi wa pembejeo bora.

Alisema hali hiyo imesababisha kuendelea kwa ununuzi wa mbolea za kwenye makopo sokoni kutokana na kushindwa kununua mbolea zilizofungwa kwenye vifungashio vya kilo 25 hadi 50 ambayo inauzwa kati ya Sh. 50,000 hadi Sh. 70,000 kulingana na aina ya mbolea.

Midyano alisema bado kuna ununuzi wa mbolea holela ambazo wauzaji wanafungua mifuko na kupima rejareja ili kusaidia wakulima wasioweza kumudu gharama za kununu mfuko mzima.

"Tunaambiwa mbolea haipaswi kufunguliwa kupigwa jua au kupimwa sokoni kwani inapoteza virutubisho vyote, lakini huwezi amini bado wakulima wananunua mbolea kwa kutumia kopo sokoni," alisema.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba serikali iwasiliane na kampuni zinazozalisha pembejeo kuzifunga kwenye kilo moja, mbili hadi tano ili kuwezesha wakulima wenye kipato kidogo kunufaika.

# Wakulima mwani wapatiwa vipande 700,000 vya kamba

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amekabidhi vipande vya kamba za manila 700,000 kwa wakulima wa mwani katika Kijiji cha Songosongo, wilayani Kilwa, mkoa wa Lindi.

Akizungumza na wananchi wa Songosongo juzi, Dk. Tamatamah alisema serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) imetoa kamba hizo, ili kuwawezesha wakulima wa mwani kwani kamba ilikuwa ni moja ya changamoto waliyokuwa wakikabiliana nayo.

Kamba hizi za manila (ambazo kila moja ina urefu wa mita 10) katika kilimo cha mwani, hufungwa katika vigingi na hutumika kwa ajili ya kuoteshea mwani ambapo mwani hufungwa katika kamba hizo zinazosaidia pia mwani kutochukuliwa na maji ya bahari pale panapokuwapo na wimbi.

Dk. Tamatamah alisema duniani kote kwa sasa mwani unalimwa kibiashara, hivyo mwani ni moja ya zao linalopewa kipaumbele katika wizara.

Katika kilimo cha mwani wakulima wanakutana na changamoto mbalimbali zikiwamo za ukosefu wa mitaji na masoko.

"Wizara kupitia sekta ya uvuvi imeanza kutoa kamba ambazo ni moja ya pembejeo muhimu kwa wakulima wa mwani ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha wakulima hao kwa kuwapunguzia sehemu ya gharama za uzalishaji ili baadaye waweze kusimama wenyewe," alisema Dk. Tamatamah.

Pia, alisema kama wakulima watalima vizuri katika kamba moja ya mita kumi katika bamvua nne (miezi miwili), wanaweza kupata kati ya kilo 8-10, na kamba hizo walizopewa zinaweza kutumika kwa mwaka mzima. Lengo la wizara ni kusambaza kamba hizi kwa wakulima wa mwani maeneo yote Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Dk. Tamatamah, ipo changamoto ya soko la mwani hasa kwenye bei kwani kwa sasa asilimia 90 ya mwani inauzwa nje ikiwa ghafi na ni asilimia 10 tu ndio inayotumika hapa nchini.

"Hivyo wizara kwa sasa inawahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili waweze kukopesheka na waweze kuanzisha viwanda vidogo vya kuchakata mwani ili kuuongezea thamani. Hii itasaidia kupunguza kiasi cha asilimia ya mwani inayokwenda nje ya nchi ikiwa ghafi na kusaidia kuongeza ajira," alisema.

Aidha, Tamatamah alisema zao la mwani linazo faida kubwa ikiwa ni pamoja na kuongeza kipato katika jamii za maeneo ya pwani hasa kwa kinamama, inaondoa umaskini lakini pia linaingiza fedha za kigeni.

Naye mkulima wa mwani, Mbimbisa Omary, alimshukuru Katibu Mkuu kwa kuwaletea vitendea kazi kwa ajili ya kilimo cha mwani.

Mbimbisa alisema kilimo cha mwani kinawasaidia mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuwasomesha watoto, kununua chakula pamoja na ujenzi wa nyumba.

Jaka Farahani, mkulima wa mwani, alisema changamoto ya masoko inawasumbua sana hasa pale wanunuzi wanaowategemea wasiponunua, hivyo aliiomba wizara kuwasaidia kutatua changamoto hiyo.

Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji (WMUV), Dk. Nazael Madalla, alisema wizara kupitia idara yake inaendelea kuhamasisha kampuni kuendelea kuchukua leseni kwa ajili ya kununua mwani na mpaka sasa zipo kampuni 7. Lengo la kuwa na kampuni nyingi ni kuongeza ushindani hivyo kampuni zinahamasishwa kujisajili ili zitambulike na ziweze kufanya biashara ya mwani.




Mkurugenzi Mkuu wa TBL Plc, Philip Redman (kushoto), akipokea cheti cha shukrani kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania, Hisham Hendi, kutokana na kushirikiana kibiashara wakati alipofanya ziara makao makuu ya kampuni hiyo yaliyopo Ilala jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 128/- zajenga nyumba za walimu

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WANANCHI wa kijiji cha Tulole kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Kahama, wamejenga nyumba mbili za walimu katika Shule ya Msingi Ntungulu zenye thamani ya Sh. milioni 128.

Ujenzi wa nyumba hizo umewezesha kuondoa adha ya walimu kusafiri umbali mrefu kufika shuleni hapo.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Mashauri Katunzi, alibainisha hayo juzi wakati akisoma risala ya ujenzi wa nyumba hizo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla hiyo iliyofanyika katika viwanja vya shule hiyo.

Alisema ujenzi wa nyumba hizo, ulianza mwaka wa fedha 2018/19 na kukamilika Oktoba 19, mwaka huu, huku wananchi wakichangia Sh. 19,616,000 na Halmashauri ya Mji Sh. 108,585,480.

Katunzi alisema kabla ya kujengwa kwa nyumba hizo, walimu walikuwa wakiishi kwenye nyumba za udongo ambazo zilikuwa hazina usalama kwao na kwamba uwapo wa nyumba hizo itasaidia walimu kuongeza kasi ya ufundishaji na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Pia alisema shule hiyo ina upungufu wa matundu ya vyoo 16 ilhali mahitaji ni matundu 24 na yaliyopo ni matundu manane tu. Alisema hatua hiyo inawafanya wanafunzi na walimu kupata adha katika matumizi ya vyoo.

Sambamba na hayo, alisema shule inakabiliwa na upungufu wa walimu wa kutosha, kusababisha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kuwa chini. Alisema shule hiyo ina uhitaji wa walimu 12 wakati waliopo ni saba.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri wa Mji wa Kahama, Clamence Mkusa, alisema halmashauri itaendelea kuwatengenezea watumishi mazingira bora ya kufanyia kazi kwa kuwajenga nyumba za kuishi hasa katika shule zilizoko maeneo ya pembezoni mwa mji ambako hakuna nyumba za kupanga.

Naye Ofisa Elimu Msingi, Anna Kiya, alisema walimu wakikaa kwenye mazingira mazuri itawasaidia kuongeza ufaulu na wanafunzi na kuwafanya kutulia kwenye vituo vyao vya kazi na kuendelea kufundisha kwa kiwango kinachohitajika.

Macha ambaye ni mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa nyumba hizo, alisema walimu wanapaswa kuzitunza kwa kuwa wazazi na serikali wametumia nguvu na fedha kuzijenga ili waendelee kutoa elimu bora kwa watoto wao.

ama
ALHAMISI OKTOBA 22, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Waogesha mabinti dawa mapenzi kuvutia wawekezaji katika ndoa**



Ukurasa 13

Kilimo tumbaku; uchumi wa kimkakati unaokwazana na adha ya mazingira, afya



Ukurasa 14

**Ushuhuda Siku Mtoto wa Kike kwa 'madudu' Kata ya Tandale**

# Wapaza sauti ukatili wa jinsia bado umo katika afya ya mama

**Na Sabato Kasika**

BEATRICE Ezekiel, ni mwanaharakati na mwelimshaji anayetamka kauli kwamba "wanawake wakiachana na uvumilivu huu, watakuwa wamejikomboa kutoka katika makucha ya ukatili wa kijinsia ambao baadhi yao wanakumbana nao kwenye ndoa."

Anawaambia wanawake wenzake wabadilike na kuchukua hatua za kisheria kukomesha vitendo hivyo kwenye ndoa zao, sauti anayopaza kwenye semina hiyo iliyofadhiliwa na Jukwaa la Vijana Wanaharakati (YFF) kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na wadau husika.

"Ukatili wa kijinsia ni kitendo anachofanyiwa mtu yeyote mwanamke au mwanamume kwa lengo la kumdhuru au kumuumiza kisaikolojia, kimwili, kiafya, kingono na kiuchumi," anasema Beatrice.

Mwezeshaji huyo anasema, utafiti unaonyesha kuwapo wanawake waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili wa kijinsia, baadhi hawavichukulii hatua.

Anasema hofu ya kuachwa na kutojiamini, imo katika orodha ya sababu zinazochangia wanawake kuendelea kuvumilia ukatili wa kijinsia kwenye ndoa, bila ya kuchukua hatua kuwanusuru katika shida hizo.

Beatrice anataja sababu nyinginezo, ni hofu na aibu katika jamii ikiwamo ukahaba na endapo wataachika, pia kuna hofu ya kutoa nje siri za familia, kutofahamu sheria, mshikamano duni uliopo katika familia, hofu ya mtazamo wa watu, usalama na utegemezi wa kiuchumi.

Pia, anafafanua kuwa wanawake wanaofanya vitendo hivyo wanatakiwa kufuata sheria, ikiwamo kwenda kwenye Dawati la Jinsia Kisheria; badala ya kuendelea kuvumilia ukatili.

Anasema, katika mazingira ya aina hiyo, uchumi wa familia huwa unayumba kutokana na mwanamke kuwa duni kiafya na kuna wakati pato la taifa linaathiriwa kutokana na mchango wa uzalishaji wa mwanamke kupungua.

"Utafiti wa kitaifa wa taasisi ya Tanzania Demographic and Health Survey (TDHS) wa mwaka 2010 unaonyesha kuwa asilimia 44 ya wanawake wote walioolewa wameshapata ukatili wa kimwili na kingono kutoka kwa wenzi wao," anasema.

Ni utafiti unaobainisha asilimia 15 ya wanawake nchini hawatiliwi maanani katika ngazi ya familia, hata kusababisha matukio hayo yaendelee kuwapo.

Anasema kuna wakati mwanamke anaweza kufanyiwa ukatili wa kiafya, ambao ni pamoja na kukosa haki ya uzazi mahali salama au mume kumnyima mke fedha za ya kwenda hospitali.

"Wapo baadhi ya wanaume wanaowazuia wake zao kutumia uzazi wa mpango, matumizi ya mipira ya kiume (kondomu), ama mwanamume kupima VVU na UKIMWI na kumficha mkewe matokeo," anasema.



Mwezeshaji Beatrice Ezekile, akiendesha darasa la elimu jinsia. **PICHA: SABATO KASIKA**

Mama huyo anaeleza kimamama wenzake wanafanyiwa mengi na lipo kundi la wanaokaa kimya wanakivumilia tu, hali inayosababisha vitendo vya ukatili kuendelea katika ndoa na ndami ya jamii.

Janeth Komba, mshiriki wa semina hiyo ya kuwanoa wadau na wanaharakati jinsia, aliwakumbusha wanawake kwamba ukatili jinsia ni jambo lolote analofanyiwa mtu hali yake na kumuathiri.

"Anaweza kuwathiriwa katika mwili, kiuchumi, kisaikolojia, kingono na hata ukatili wa mtandaoni. Hivyo, wanawake tusinyamazie vitendo hivyo, badala yake tuchukue hatua zinazostahili ili kukomesha hali hiyo," anasema Janeth.

Mwanamama Zahra Omary, anasema Tanzania imeridhia mikataba ya haki za binadamu na kupinga ukatili wa kijinsia na kwamba ukatili wa kijinsia ni ukiukwaji wa haki za msingi za binadamu.

"Tanzania imesaini mikataba ya haki za binadamu ili kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake, ikiwamo ya Beijing na Maputo ili kutimiza lengo namba tano Maendeleo Endelevu," anasema.

Anasema, lengo linahusu kuendeleza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana na kwamba Katiba ya nchi inatamka kila binadamu anastahili kuheshimiwa na kupewa hadhi.

AFYA

# Waogesha mabinti dawa mapenzi kuvutia wawekezaji katika ndoa

- Shida nini? Kuinasa mahari ng'ombe
- Maelekezo: Kosea mtihani, shule iishe
- Uzazi mpango bado kitendawili tata

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MILA na desturi katika Mkoa Shinyanga inatajwa kuwa chanzo cha wanafunzi wa kike wenye umri kushindwa kuhitimua elimu ya msingi na sekondari.

Hapo wanaotajwa hasa wenye umri miaka 16 hadi 20, kwa wazazi kuwaozesha wakiwa bado masomoni, hofu ikiwa kinachotajwa hata wakaozeshwa pasipo umri na wakati sahihi, dai kuu ni "anaweza kuharibika akiwa mikononi mwake."

Ili kuachana na hilo, mbadala wao wanaoamini ni busara ni wa kumtafutia mtoto mume na ili kukwepa kuendelea na masomo, mtoto anashawishiwa afanye vibaya kwenye mitihani ya mwisho.

Wengine wamewaozesha watoto vilabuni kwenye pombe, bila ya mzazi wa kike kufahamu, wameshakubaliana ng'ombe, huku mila husika inataja mzazi wa kike hana haki ya kuhoji kinachoamuliwa.

Ili kufanikisha hilo, wazazi hao huozesha mabinti, wakianza kwa kuwapeleka kwa waganga wa jadi, wanawaogesha dawa za mvuto wa mapenzi, wanachanjwa, lengo ni kuwezesha kupata mchumba haraka.

Aidha, kuna madai waganga wa jadi wamekuwa wakitumia fursa hiyo kudanganya vijana wenye umri wa kuoa, hasa anapopata binti wa kumwogesha dawa za mapenzi kwa lengo la mahari ya ng'ombe, huku katika upande wa pili. mzazi anayekubali bintiye kuogeshwa, hutafutiwa vijana wenye uhitaji na mke.



Mwezeshaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Rehema Mwateba, akiendesha mafunzo ya ujenzi wa nguvu ya pamoja kuimarisha mila na desturi chanya kwa wasichana wa kata za Shilela na Lunguya, Halmashauri ya Msalala. Picha ya chini ni ng'ombe, mali inayotawala kuvutia ndoa za utotoni. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

### WASHIRIKI/WANANCHI

Sasa inaelezwa, hilo limeshtukiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ulioamua kuchukua jukumu la kuandaa nguvu ya pamoja kuimarisha mila na desturi chanya, kupingana na nyendo za mikla hizo, Nipashe ikishuhudia imeanza kufanyika katika kata kama za Shilela na Lunguya.

Lameck Kanyefu, mkazi wa kata Shilela, ana ushuhuda wa madai hayo ya wazazi kuozesha mabinti zao, wakipitia kwa waganga wa jadi kuwaogesha dawa za mvuto kimapenzi.

"Anathamini sana ng'ombe kuliko kitu chochote kile. Wakati wa mahari ya kumuoza binti hata ukimpatia Sh. milioni 10 hatajisikia vizuri na ndio sababu wafugaji wengi wa jamii yetu kuwaozesha watoto wao kwa mifugo," anaeleza Kanyefu.

Hamisa Hamis, ana ufafanuzi kwamba kwenye familia wamekuwa wakielewana thamani ya mahari wakiwa kwenye vilabu vya pombe na mama baadaye anapewa taarifa, pasipo fursa ya kuhoji yatokanayo.

Mkazi wa Lunguya, Irene Nyanza, ana maonji kwamba, mabinti zao wamekuwa wakikosa furasa za masomo, kwa mbadala wa mzazi kuendekeza kitega uchumi cha ng'ombe itokayo na binti kuozeshwa.

Kutokana na hilio, ana ushauri kwamba elimu inayohusu mila potofu, inatakiwa kutolewa chini ambako kuna waathirika wengi.

Kuna dhana imejengeka vichwani mwetu kuwa mtoto wa kiume anaposoma na kupata kazi, ndiyo atakayekuja kusaidia familia na mtoto wa kike hawezi kusoma na akiolewa atakwenda kuisaidia na kujitoa kwenye familia aliyoolewa," anasema.

### WATEKELEZAJI SHERIA

Lusajo Manase, ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lunguya, anasema baadhi ya viongozi wao, hasa wenyeviti wa vitongoji na vijiji, wamekuwa wakishiriki katika uozeshaji wa mabinti wadogo chini ya umri miaka 18, akirejea ushuhuda wa kuwa wageni rasmi kwenye sherehe za ndoa hizo.

Anasema, kuna madai viongozi hao wa ngazi ya chini hushirikishwa katika mchakato wa uozeshaji huo, kwa 'bakshishi' ya kupatiwa ng'ombe iwapo uozeshaji utakanilika pasipo kelele au kasoro.

Manase anaelezwa hatua zao, kwamba wamekuwa wakivunja ndoa nyingi na kuwachukulia hatua za kisheria wote wanaohusika moja kwa moja, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola, pale wanapopatiwa taarifa kutoka kwa wasamaria wema.

Pia, ana ushauri kwamba, viongozi wa madhehebu ya kidini kwenye ibada zao waendelea kutoa elimu ya madhara ya ndoa za utotoni kwa waumini, kuwapo mabalozi wazuri katika nyumba zenye hofu ya Mungu.

### FAMILIA ZINAKIMBIWA

Ndalahwa Mathius, Mhudumu wa Afya Ngazi ya Jamii, aliyeko Msalala, anaibuka na hoja nyingine tata kwamba kuna wanaume wanaotelekeza familia zao baada ya wake zao kushindwa kufuata uzazi wa mpango au kufunga kizazi.

Inadaiwa kwamba, kinamama hao wanaacha kudhibiti kizazi, wakilitekeleza hilo kama sehemu ya hofu kinamama hao hawafungi kizazi, kuhofia waume zao huenda watatafuta mke mwingine na kuendelea kuzaa.

Anaeleza uzoefu uliopo ni kinamama ndani ya jamii ya makabila ya eneo hilo, wengi wametelekezewa familia na waume zao, baada ya kuzaa mfululizo, wakikiuka uzazi wa mpango.

Mathius anasema, kwasasa kinamama wanashindwa kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za uzalishaji mali kwenye familia zao, ikiwamo kilimo baada ya uwepo wa familia kubwa na kusalia kulea wingi wa watoto alio nao.

"Tumekuwa tukiwapatia elimu ya uzazi wa mpango wa muda mrefu na mfupi, kama atashindwa kitanzi au kipandikizi anatakiwa kutumia kondomu au sindano ili kuepuka kuendelea kuzaa kila mwaka na kuondoa dhana ya kukimbiwa na waume zao," anasema Mathius.

Mama Irene Nyanza, analalamika kwamba waume zao wanapenda sana kuzaa, lakini inapotokea wingi wa watoto, huwa mstari wa mbele kukimbia majukumu walio nayo, wakiwa mbadala wa kuwa na mwanamke mwingine akiendeleza ya awali.

Hata hivyo, anaasa kwamba wameshaanza kuchukua hatua ya kiafya, kwa kufunga kizazi cha kinamama kwa njia ya siri na hasa pale waume zao wanapokuwa safarini, lengo ni kusimamisha rasmi kuzaa, mama hao wapate fursa ya kushiriki kuzalisha malii.

### MKONO TGNP

Mwezeshaji kampeni kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Rehema Mwateba, anasema kumuoza mtoto wa kike mwenye umri mdogo ni hali ambayo kiafya inasababishia baadaye asipate uzazi, baada ya mbegu zinazosababisha mimba kutofika sehemu husika ya uzazi, vinavyoishia kuharibika.

"Hata Mimi nilikuwa mmoja wa wahanga niliyezaa watoto mfululizo tangu mwaka 1979 hadi 1980 na aliyenishauri juu ya uzazi wa mpango wa kuzaa kwa hatua, alikuwa ni baba yangu mzazi, maana ningekosa hata muda wa kufanya shughuli za uzalishaji," anafafanua Mwateba.

Anakumbusha, mama anapojifungua watoto mfululizo bila kufuata uzazi wa mpango, unaunda familia kubwa inayokosa muda wa kuihudumia.



MAZINGIRA

# Kilimo tumbaku; uchumi wa kimkakati unaokwazana na adha mazingira, afya

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TUMBAKU iko katika orodha ya mazao makuu manane ya mkakati kibiashara yanayozalishwa nchini na kuliingizia taifa fedha nyingi, hasa za kigeni.

Ni mazao ambayo yakitajwa, moja kwa moja inaguswa 11 nchini ambayo ni Shinyanga, Kagera, Geita, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Morogoro, Iringa, Ruvuma Mara na 'gwiji' lao Tabora, ambayo takwimu za Wizara ya Kilimo, inaitaja kuongoza kwa kuzalisha asilimia 50 ya tumbaku yote nchini.

Pia, takwimu hizo zinadokeza mabadiliko ya uzalishaji katika kipindi cha miaka mitano kuanzia msimu wa mwaka 2015/2016.

mpaka 2019/2020 kutokana na sababu mbalimbali.

Zinaonyesha kuwa msimu wa 2015/2016 zilizalishwa tani 60,619, msimu wa 2016/2017 zilizalishwa tani 58,639, msimu wa 2017/2018, zilizalishwa tani 50,522, Msimu wa 2018/2019 zilizalishwa tani 70,824 na Msimu wa 2019/2020 zilizalishwa tani 70,087.

Pamoja na mabadiliko hayo, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inataarifu bado iko juu katika kuliigizia taifa fedha nyingi, Dola za Kimarekani milioni 1,092.90 kutokana na mauzo ya nje; pia Sh. bilioni 101.4 kutokana na mauzo ya ndani.

Hata hivyo, zao hilo la utajiri hadi sasa linakabiliwa na matatizo mengi kiasi cha kutisha baadhi ya wakulima kuanza kuogopa, ikiwamo kutetereka soko lake, kampuni wateja wake wa kudumu, nyingi zimejitoa, hata kufanya wanunuzi wachache waliobaki kutokuwa washindani.

Mteja maarufu, kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco Company (TLTC) ilijitoa kuanzia msimu wa kilimo 2018/2019, katika uzinduzi wa soko kitaifa, katika Kata ya Lupatingatinga wilayani Chunya.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa pili kulia), akisikiliza maelezo namna ya kuteua madaraja ya tumbaku, kutoka kwa Mteuzi Mkuu wa Tumbaku kutoka katika Bodi ya Tumbaku nchini (TTB), Albert Chale, wakati wa uzinduzi wa masoko kitaifa. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

### KUTOKA TTB

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku nchini (TTB), Stanley Mnozya, anasema soko la tumbaku inapitia misukosuko tangu msimu wa kilimo 2014/2015.

Anasema moja ya sababu zinazokimbiza kampuni za ununuzi wa zao hilo, ikiwamo TLTC, ni wingi wa kodi kwenye Soko la Tanzania, anayesema wanunuzi wengi walikimbilia nchi za Malawi na Zimbabwe.

Mnozya anazitaja sababu zingine wanunuzi hao kukimbia soko la Tanzania kuwa ni wakulima kukiuka taratibu za kilimo hicho ikiwamo kutopanda miti ya kukaushia zao,pamoja na kuajiri watoto kwenye shughuli hiyo.

Hata hivyo Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ambaye ndiye aliyezindua masoko hayo, anasema kutokana na faida ya zao hilo, Serikali inaendelea kutafuta masoko katika mataifa mbalimbali duniani, ikiwamo China na Misri.

Rai yake ni wakulima kuendelea kufuata taratibu za kilimo cha zao hilo na TTB kuwasajili wakulima wote wa zao hilo, ambalo ni sehemu ya kipaumbele kitaifa.

### VITA VYA AFYA

Matumizi ya tumbaku na mazao yake yamekuwa yakipigwa vita na baadhi ya taasisi na wanaharakati wa afya, kwa madai ya kusababisha magonjwa mbalimbali yakiwamo kansa, kifua kikuu (TB) na mengine ya njia ya hewa.

Shirika la Afya duniani (WHO), limo katika wanaopinga matumizi ya tumbaku duniani, ikiwa imetua siku ya Mei 31 ya kila mwaka kuwa maalumu ya kupinga matumizi hayo.

Taarifa ya WHO ya Mei mwaka jana, inasema watu milioni nane hufariki dunia kila mwaka kutokana na madhara ya tumbaku na mamilioni engine wanaishi na magonjwa yatokanayo na matumizi yake.

Vilevile taarifa hiyo inaonyesha watoto 60,000 wenye umri wa chini ya miaka mitano hufariki kila mwaka, kutokana na athari za kuvuta moshi wa watu wanaovuta tumbaku, ikitamka matumizi ya tumbaku ndiyo chanzo pekee cha ugonjwa wa saratani kinachozuilika.

Kitendo cha WHO kupinga matumizi ya zao hilo, kinachochea watumiaji sasa kupungua na inaeleza uwezekano wa kilimo chake kuanza kushuka pia.

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya mwaka 2017, Rehema Madusa, kuna wakati aliwashauri wakulima tumbaku wilayani humo kuanza kuzalisha mazao mengine ikiwamo korosho na alizeti ili kujiandaa kuachana na kilimo cha zao hilo.

### UHARIBIFU MAZINGIRA

Kilimo cha tumbaku ni miongoni mwa shughuli zinazodaiwa kuhitaji mvua za kutosha, huku yenyewe haiku rafiki kwa vyanzo vya mvua, ikiwemo misitu na inachochea ukataji wmiti kwa ajili ya uzalishaji wake.

Inaelezwa kitaalamu, kilimo tumbaku kinachochea ufyekaji misitu kwa ajili ya kuanzisha mashamba mapya, vitalu vya zao hilo, usafirishaji na hata kuni kwa ajili ya kukaushia.

Mwaka 2016, aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha wakulima wa Tumbaku wa Kijiji cha Igagwe (Igagwe Amcos) cha wilayani Chunya, Gulila Mwakosya, alitoa taarifa iliyoonyesha kuwa asilimia 75 ya uzalishaji wa tumbaku inategemea matumizi ya miti.

Kiongozi huyo anasema, ukaushaji tumbaku wastani wa ekari moja ya shamba, unahitaji tani mbili za miti na kwamba kiasi hicho cha kuni ni kwa majiko ya kisasa, ambayo yasiyotutumia kuni nyingi, lakini majiko ya kienyeji yanahitaji kuni zaidi.

Wanaharakati wa mazingira, wamekuwa wakipinga kilimo hicho kuendelea ili kuokoa misitu na katika kukabili uzalishaji wake, serikali ilianzisha utaratibu wa kuwalazimisha wakulima kila mmoja, pia na 'Amcos' kupanda miti.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa TTB, Mnozya ni kwamba bodi hiyo imeanza kuwaondoa kwenye daftari la usajili wakulima wote wanaoshindwa kutekeleza agizo la kupanda miti.

### USALAMA WA WATOTO

Baadhi ya vitendo vya walima tumbaku, vinadaiwa kuwana vitendo vinavyokinzana na baadhi ya sheria zinazosimamia ajira ikiwemo, ikiwamo kuhusu ajira ya mtoto, huku Shirika la Kazi duniani (ILO), ikibeba ripoti inayogusa uwapo wa watoto milioni 4.2 duniani wanaotumikishwa kwenye shughuli mbalimbali, ikiwamo mashambani.

Aidha utafiti uliofanywa hivi karibuni na Shirika lisilokuwa la kiserikali Winrock International kwa kushirikiana na serikali, ulibaini zaidi ya watoto 4,200 nchini wanatumikishwa kwenye shughuli mbalimbali na wengine wanaishi kwenye mazingira hatarishi.

Hivi karibuni Winrock kupitia mradi wake wa Prosper lilifanya shughuli ya kuwaondoa watoto wanaotumikishwa mashamba ya tumbaku kwenye mikoa ya Mbeya, Songwe na Tabora, wakunua kuwafikia walengwa wastani 600.

Mlolongo wa matatizo ya kiutendaji na mabadiliko ya hali ya hewa, yamekuwa yakisababisha kudorora soko la zao hilo, hasa mvua inaponyesha kupita kiasi, ukaushaji tumbaku unakuwa mgumu.

Serikali kwa upande wake inaendelea kuchukua hatua kubwa, ikiwamo katika tafsiri yake kuwa zao la kimkakati, mfano hai ufuatiliaji wa kiwango cha juu kuhusu kasoro zinazojitokeza kukwaza soko la uzalishaji uliopo.



Kilimo cha tumbaku kikiendelea shambani. **PICHA: MAKTABA.**

AFYA

# Ushuhuda Siku Mtoto wa Kike kwa 'madudu' Kata ya Tandale

**Na Beatrice Philemon**



Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kwa Tumbo Tandale, Kibwana Khatibu (aliyesimama).

SIKU ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike Duniani, inawahimiza vijana wa jinsia zote kuanzia umri miaka 16, wanaaswa kutumia vituo vya afya, vinavyotoa huduma rafiki za afya ya uzazi.

Kuna sababu kuu inayotajwa ni kupinga mimba za utotoni, vifo vya mabinti na upatikanaji taarifa sahihi kuhusu huduma za afya.

Katika hilo, vijana wanahimizwa kutumia vituo tajwa, kwa sababu vinatoa mafunzo na ushauri kwa vijana kuhusiana na elimu ya afya ya uzazi, athari dawa za kulevya, kinga dhidi ya mimba za utotoni, pia kupatikana taarifa sahihi za huduma ya afya.

Mafunzo mengine, ni madhara ya mimba za utotoni, ushauri kuhusu uzazi wa mpango, kutambua tiba ya magonjwa ya viungo vya uzazi, ikiwamo elimu ya Ukimwi.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike Duniani, Meneja Mradi wa Chama cha Wanawake Vijana wa Kikristo Tanzania (YWCA) Idda Swai, ana ufafanuzi:

"Hivi sasa YWCA kwa kushirikiana na wadau wengine wameanza kuhamasisha vijana kutumia huduma rafiki katika vituo vya afya vilivyoko katika maeneo yao, ili kupinga mimba za utotoni na kuleta mabadiliko chanya kwa vijana."

Ni namna ya kuhamasisha huduma rafiki kwa vijana, ili kupinga mimba za utotoni unaotekelezwa kupitia mradi unaoitwa 'Afya Yetu Malengo Yetu' ukifadhiliwa na asasi kimataifa isiyo ya kiserikali inayoitwa Deutsche Stiftung Weltbevölkerung (DSW).

Mradi huo wa miezi sita unatekelezwa na YWCA na DSW wilayani Kinondoni, ikitajwa kigezo kikuu ni kuwapo vituo vingi vya afya na vijana wengi hawafahamu afya ya uzazi.

Hiyo inaelezwa kuwa mahali sahihi pa kupata taarifa bora kuhusu mabadiliko ya miili na changamoto zinazowatokea katika umri wa kupevuka na baadhi hawaelewi kwa kina, maisha na elimu kuhusu magonjwa zinaa na madhara yadawa za kulevya.

"Tumechagua wilaya ya kinondoni kufanya uhamasishaji vijana waweze kutumia vituo vya huduma rafiki, ili kupinga mimba za utotoni kwa sababu 'patners' (wenza) wetu mpango kazi wao upo wilaya ya Kinondoni.

"Huu ni mradi wa miezi sita na umelenga kufikia vijana 300,kupitia maadhimisho haya tuweza kuelimisha vijana zaidi ya 100," anasema, huku akiwaomba vijana watumie yote wanayofunzwa na kutumia vituo vya afya, ili wapata taarifa sahihi.

**MABINTI NA SAYANSI**

Mratibu Afya ya Uzazi na Mtoto, Manispaa ya Kinondoni, Edith Mboga, anawaasa vijana kuweka malengo katika maisha yao, huku wakiepuka mimba za utotoni.

Anawakumbusha wasichana kujituma hasa katika masomo ya sayansi, ikiwa namna ya kupinga kwa vitendo dai 'ni fani ya mtoto wa kiume.'

"Tuweke malengo katika elimu na kufika ngazi ya chuo kikuu, ukimuelimisha mtoto wa kike unaelimisha jamii, familia na taifa kwa ujumla na mkiwa shuleni musome sana masomo ya sayansi ili ukiamua kuwa daktari, mfamasia, mbunge, mhandisi uwe mwalimu bora au mtaalamu bora," anasema

Mbali na hilo, alimshukuru Rais John Pombe Magufuli kwa kuanzisha elimu bure kuanzia shule ya msingi na sekondari, hivi sasa shule zimeongezeka na nafasi zimeongezeka.

Inaelezwa, mpaka sasa mkoa Dar-es Salaam una jumla ya vituo 67 vya kutoa huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana na kati ya hivyo, 27 ni vya serikali,

"Mnapokuwa vijana, vituo vyetu vinatoa huduma bora, njoo kwenye vituo vya afya, sisi tutatoa elimu sahihi ili mpate huduma sahihi na muwe na afya bora," anasema

**KILICHOJIRI TANDALE**

Ofisa Ustawi wa Jamii katika Zahanati ya Tandale, Ainess Charles, anasema kata hiyo ni miongoni mwa kata inayokumbana na changamoto kubwa kutoka kwa vijana, hasa akitaja mimba za utotoni, pia wanaobakwa na ukatili wa kijinsia.

"Sisi kwa kushirikiana na serikali na YWCA, tupo kwa ajili ya kuelimisha jamii ili kujua ukatili wa kijinsia, madhara ya ukatili wa kijinsia, kwa sababu katika Kata ya Tandale, watoto wanabakwa sana na kinamama kufanyiwa ukatili wa kijinsia," anasema.

Ombi lake analiliekeza kupitia tukio la kutebelewa, ni kwamba vijana wake wakala bora wa kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia katika maeneo yao, ili wasaidiwe kupata haki zako.

"Pia, ukiona kuna mtoto au mtu mzima amefanyiwa ukatili wa kijinsia wape mwelekeo waje katika eneo hilo kumsaidia, awe mtoto, babu, mama, ili kuzuia ukatili wa kijinsia kwa watu wote na namba ya kupiga ni 116 kuripoti ukatili huo," anasema

Mkasa wa kumshamiri ubakaji Tandale wapangaji katika nyumba mbalimbali wanadaiwa kuwa vinara wa vyote; upangaji na ulawiti.

Ainessa, anafafanua namna kunavyokuwapo ukatili wa kimwili, analalamika kila wiki anapata mikasa kesi 10, nusu kinamama na waliobaki watoto.

Ofisa huyo anasema, waathirika zaidi ni watoto wenye umri kati ya miaka 16 hadi17, akitaja vyanzo vikuu ni hasa za hela ndogo anazozibatiza 'Sh. 200' na huduma za bodaboda.

Anasema hivi sasa wataalamu kutoka kituo cha afya cha Tandale wameanza kwenda kwenye jamii na kuelimisha watu kuhusu ukatili wa kijinsia ili kupunguza tatizo la ukatili wa kijinsia.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Tandale, Khatibu Kibwana, anayekubaliana na kuwapo machafu hayo mahali alipo, anawahamasisha vijana Tandale kwenda kwenye vituo vya afya kupata mafunzo na taarifa sahihi.

"Mimba za utotoni zinaleta vifo, magonjwa ya zinaa, ukimwi na maradhi mengine," anasema Kibwana, anayefafanua kwamba Tandale kuna majanga mengi hivi sasa, ikiwamo mabinti wanapakizwa kwenye magari kufanya mbwembwe za kimuziki zisizo na staha, badala ya kusoma.

"Mtoto wa kike itambue thamani yako kama kijana, ili maisha yenu yaendelee na muweze kutimiza ndoto zenu," anasema.

Ofisa Mtendaji Tandale, Kibwana, bawa Kata ya .... anayeishukuru YWCA na DSW kuwahudumia katikia siku ya mtoto wa kike, anainisha Kata Tandale ina wakazi zaidi ya 70,000, wengi ni wenye kipato cha chini kiuchumi.

"Hivi sasa tunahamasisha wananchi wafikie angalau maisha ya kati hasa kwa upande wa elimu na sasa hivi tukikuta unampa mtoto wa kike mimba 'tuna - deal' (kushughulika) na wewe naomba pia Ofisa Maendeleo na Mganga Mkuu, tushirikiane kwa jambo lolote," anasema



Mafunzo kwa vijana kujihami dhidi ya maradhi, yakiendelea katika Zahanati ya Tandale, Dar es Salaam. Aiiyekaa mbele ni Ofisa Ustawi Jamii wa zahanati. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**



# CPB yaanzisha mkakati kufufua kilimo cha ngano

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko nchini (CPB), imeanzisha mkakati wa kufufua kilimo cha ngano Kanda ya Kaskazini ili kuondokana na uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

Pia, serikali inatumia Sh. bilioni 530, kuagiza tani 800,000 za ngano kutoka nje ya nchi kila mwaka. Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Nafaka na Mazao mchanganyiko, Valerian Mablangeti, aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi unatokana na kudorora kwa kilimo cha ngano nchini kwa viwanda vingi kuagiza kutoka nje.

"Kutokana na hali hiyo bodi ilianza uhamasishaji wa kilimo cha mkataba katika maeneo ya West Kilimanjaro, Mbulu, Karatu na Hanang baada ya Naibu Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, kutembelea wakulima wa maeneo hayo mwezi Agosti, mwaka huu," alisema Mablangeti.

Alisema lengo la mpango huo ni kuhakikisha mahitaji ya kiwanda tani 36,000 kwa mwaka yanapatikana kutokana na kilimo hicho pia kuhamasisha zaidi wakulima kuwauzia waendesha viwanda wengine.

"Hadi sasa baadhi ya wakulima wa West Kilimanjaro tayari wameshasaini makubaliano ya kilimo cha mkataba kuanzia mwezi Machi 2021, na timu ya wataalamu wa CPB, wanaendelea na zoezi la kukamailisha mazungumzo na kusaini mkataba wa wakulima wa Mbulu, Karatu na Hanang," alisema.

Alisema, hatua hiyo inakwenda na kuhamasisha uundwaji wa vikundi vya wakulima, kusajili wakulima na uhakiki mashamba ya wakulima wa ngano katika maeneo tajwa.

Alifafanua kuwa, ili kuwawezesha wakulima kufanikisha azma ya kilimo cha ngano, CPB inashirikiana na benki kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kupata mikopo.

"Bodi pia imeshirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) na Taasisi ya Uzalishaji Mbegu (ASA), kwa ajili ya kupata mbegu bora," alibainisha.

Hata hivyo, alisema kuwa Shirika la Bima la Taifa (NIC), linashiriki katika mpango huo ili kutoa bima ya mazao shambani kwa wakulima ili pamoja na mambo mengine kuwawezesha kupata nafuu katika mikopo ya benki. "Kwa mikakati tuliyojiwekea sisi bodi ni kufika uzalishaji wa tani 400,000 katika kipindi cha miaka minne ijayo ili kuondokana na matumizi ya fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa hii nje ya nchi na fedha hizo kufanya mambo mengine," alieleza Mablangeti.



Wanakikundi cha Tupendane cha Chikola, kinachojishughulisha na kilimo cha zabibu, nyanya na mboga wakiangalia maeneo yao yanayotumika kwa shughuli za mashamba ambayo hivi sasa yamevamiwa na wachimbaji wa mchanga na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, katika Mtaa wa Kisisiri, Kata ya Matumburu, Wilaya ya Dodoma, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watanzania watakiwa kuwa makini siku ya kupiga kura

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kuwa makini siku ya kupiga kura za kuchagua viongozi katika uchaguzi mkuu, wiki ijayo ili kuepuka makosa ya kuwachagua wasiowajua.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Dodoma, Ahadi Sinene, alitoa kauli hiyo juzi wakati alipozungumza kwenye mkutano wa kampeni wa kuwanadi wagombea wa hicho uliofanyika Kata ya Mbambala, jijini hapa.

Sinene, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi siku ya upigaji kura na kuweka umakini katika zoezi hilo muhimu la uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu.

"Ndugu zangu hakikisheni mnakuwa makini siku ya kupiga kura ili kuepuka kuweka kura yako kwa mgombea usiyemjua, angalia vizuri nembo ya chama na sura mgombea wako ili kuepuka kukosea," alisema.

Alisema kama kuna wazee au wale wasiojua kusoma na kuandika, wanatakiwa kuwachagua watu wa familia yao au wanayemwamini ili asidanganywe na kupoteza kura yake.

Pia aliwataka wananchi kuwachagua wagombea wa chama hicho ambao ni mgombea urais kupitia chama hicho, John Magufuli na Mbunge Anthony Mavunde.

Alisema serikali imefanya mengi na wakiichagua itaongeza hatua zaidi kwenye maendeleo.

Vile vile, alisema katika miaka mitano wamejenga madarasa, barabara na huduma za afya kila wilaya na katika ilani ya uchaguzi ya CCM mwaka huu watasaidia kukuza uchumi zaidi.

Aidha, Sinene aliwataka wananchi kuandaa vitambulisho vya kupigia kura ili kuwa na uhakika wa kwenda kupiga kura na kumchagua kiongozi atakayewaongoza kwa miaka mitano.

Kwa upande wake mgombea udiwani wa CCM Kata ya Mbambala, Pascazia Mayala, aliwaomba wananchi kumchagua tena ili akamilishe mipango ya maendeleo waliyojiwekea.

Alitaja baadhi ya mafanikio yaliyofanyika wakati wa uongozi wake kuwa ni uchimbaji wa visima kila kijiji kutokana na misaada kutoka serikalini na wafadhili mbalimbali.

Alitaja mambo mengine kuwa ni kuanzishwa kwa vikundi 27, vya kinamama na 22 vya vijana ambavyo vyote vilifanikiwa kupata mikopo ya fedha kwa ajili ya maendeleo kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

## Mwekezaji Ranchi ya Kikulua aongezewa mkataba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMPUNI ya Ranchi za Taifa (NARCO), imemwongezea mkataba mwekezaji wa Ranchi ya Kikulua, mkoani Kagera baada ya kufanya vizuri katika uwekezaji wa awali.

Awali, mwekezaji huyo alikuwa na mkataba mfupi na baada ya NARCO kuona amefanya vizuri imemwongezea mkataba wa muda mrefu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Meneja Mkuu wa NARCO, Masele Mipawa, alisema baada ya kutembelea ranchi hiyo na nyingine na kufanya tathmini wameona anastahili kuongezewa muda wa uwekezaji ili kuboresha huduma za utoaji bidhaa zitokanazo na nyama.

"NARCO tuko makini kuhakikisha kila mwekezaji anafanya vizuri katika ranchi ambayo amepewa kufanya kazi, akifanya vizuri anaongezewa," alisema.

Masele alisema mwekezaji wa Kikulua ameonyesha yuko bora katika idara zote hususani kwenye uchinjaji, ufugaji na utoaji wa bidhaa nyingine kama maziwa.

Alisema, mwekezaji huyo anastahili kuwekeza kwa muda mrefu kwa kuwa anakidhi vigezo vyote vya kuwa mwekezaji wa muda mrefu.

Akizungumzia kuhusu wawekezaji wengine aliwataka kuwa makini kwa sababu NARCO inapita kila ranchi kuangalia ubora wa utendaji kazi, pia uwekezaji unaofanywa na mwekezaji.

Alifafanua kuwa, lengo lao ni kuona kila ranchi inafanya vizuri katika uwekezaji ili wanaopata huduma hiyo wapate huduma bora.

Akizungumzia mipaka, alisema wanajitahidi kuhakikisha wanaondoa migogoro baina ya mkulima na mfugaji.

Alisema lengo ni ranchi zao zote kufanya kazi vizuri ili kuhakikisha zinatoa huduma bora kwa jamii.

Alisema pia Bodi ya NARCO, imekuwa mstari wa mbele kufanya ziara za kushtukiza katika ranchi mbalimbali zenye wawekezaji.

Katika hatua nyingine NARCO, imejipanga kutoa huduma bora kwa jamii kutokana na kuweka mikakati ya kupitia ranchi zote ambazo zina wawekezaji.

Hata hivyo, alisema ranchi zote zinapaswa kuwa na viwango bora, ili kuwavutia watumiaji wa nyama na maziwa kuwa na imani na bidhaa zinazozalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.





# Mawakala wa vyama watakiwa kuzingatia sheria za uchaguzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAWAKALA wa vyama vya siasa na wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, jijini Mbeya wametakiwa kuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi ili kuepuka kuharibu uchaguzi.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Elias Ng'wanidako, alisema hayo jana wakati alipokuwa anawaapisha mawakala wa vyama vya siasa watakaoviwakilisha vyama hivyo kwenye vituo vya kupigia kura.

Alisema kwa mujibu wa sheria na kanuni za uchaguzi, mawakala hao ndio watakaoviwakilisha vyama hivyo kwenye vituo vya kupigia kura na ndio watakaotia saini kwenye fomu za matokeo kuthibitisha matokeo hayo.

Ng'wanidako alisema katika jiji hilo kutakuwa na vituo 760 vya kupigia kura ambavyo kila kimoja kitakuwa na msimamizi mkuu wa kituo, msimamizi msaidizi mmoja, wakala mmoja wa kila chama kulingana na wale ambao watakuwa wamewakilishwa na vyama vya siasa.

Alisema mawakala walioapishwa ni 200,092 na kwamba waliapishwa kulingana na kanuni za uchaguzi ambazo zinawataka waapishwe siku saba kabla ya siku ya uchaguzi.

"Kazi yao kubwa kwa mujibu wa maelekezo ya tume ni kwamba ndio watakaokuwa waangalizi wa kuona mwenendo wa uchaguzi na baada ya hapo watatakiwa kusaini fomu za matokeo hivyo ni watu muhimu ambao wanatakiwa kuzingatia sheria," alisema.

Mkurugenzi huyo aliwataka wapigakura kurudi nyumbani baada ya kumaliza kupiga kura ama kurejea kwenye shughuli zao za kawaida wakati wanasubiri matokeo na kwamba hawatakiwi kubaki kwenye vituo vya kupigia kura kama ambavyo baadhi ya vyama vimekuwa vikiwashawishi wapiga kura wao.

# Rushwa yakithiri vyama vya siasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imesema vyama vya siasa vimetuhumiwa kwa matukio mengi ya rushwa kuliko taasisi nyingine yoyote katika kipindi cha miezi mitatu ya mchakato wa uchaguzi mkuu kuanzia Julai, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Mkuu wa TAKUKURU wa Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema katika kipindi hicho taasisi ilipokea taarifa 263 zinazohusu rushwa.

Matechi alisema kati ya taarifa hizo, 47 zilikuwa zinawahusu wanasiasa na vyama vya siasa, huku wakifuatiwa na wafanyabiashara ambao taarifa zao zilikuwa 37 na halmashauri ambazo taarifa zake zilikuwa 36.

"Sote tunafahamu kuwa nchi yetu iko kwenye kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu, hivyo tunawakumbusha wananchi wasikubali kuuza kadi zao za kupigia kura na tunashauri kila mmoja ajitokeze kupiga kura bila kurubuniwa ili tuwachague viongozi tunaowakusudia," alisema Matechi.

Alizitaja taasisi zingine zilizotuhumiwa zaidi na idadi kwenye mabano ni ardhi (27), Mahakama (24), Elimu (23), vyama vya ushirika (16), mashirika ya umma (14) na Polisi 10.

Taasisi zingine, kwa mujibu wa Matechi, ni taasisi za fedha (saba), kilimo (tano), afya na serikali kuu (tatu kila moja), maji na biashara (mbili kila moja) habari na mapato moja moja.

"Katika kipindi hicho TAKUKURU mkoa tuliendelea na kesi 17 zilizokuwa mahakamani na tulifungua kesi mpya tatu na tulishinda kesi nne zilizotolewa uamuzi na mahakama katika kipindi hicho," alisema Matechi.

Vilevile alisema katika kipindi cha miezi hiyo mitatu, TAKUKURU iliokoa Sh. milioni 213.16 za vyama vya ushirika na vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) zilizokuwa zimefujwa na viongozi na watu wengine waliokuwa wamekopa.

Alisema fedha hizo ziliokolewa katika halmashauri zote tano za Mkoa wa Mbeya, ambapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ziliokolewa Sh. milioni 76.19, Kyela Sh. milioni 42.1, Chunya Sh. milioni 4.07, Mbarali Sh. milioni 34.45 na Rungwe Sh. milioni 56.3.

Pia alisema taasisi hiyo ilifanya uchambuzi wa mifumo sita na kufuatilia thamani ya fedha katika miradi 10 katika sekta ya maji, elimu na afya mkoani humo ili kuangalia kama inaendana na thamani ya fedha zilizotolewa na serikali.



Baadhi ya mawakala wa vyama vya siasa jijini Mbeya wakiapa jana kwa ajili ya kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

# CHAVITA yaomba elimu bidhaa feki

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHAMA cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), kimeiomba serikali kupitia Tume ya Ushindani nchini (FCC), kutoa elimu ya kuzitambua bidhaa feki kwa wajasiriamali viziwi ili kujiepusha na madhara ya kiafya na mkono wa sheria.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini hapa na Mwenyekiti wa CHAVITA Mkoa wa Mbeya, Tusekile Mwalwega, wakati wa mafunzo kwa kundi hilo juu ya utambuzi wa bidhaa feki na athari zake katika suala la uchumi na afya.

Mwalwega alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa kundi hilo kwa sababu asilimia kubwa ni wajasiriamali hivyo wakitambua bidhaa feki itawasaidia kukwepa hasara pamoja na mkono wa sheria.

"Tunaishukuru FCC kwa kutupa mafunzo haya na namna ya kutambua bidhaa feki licha ya kuwa ni kundi dogo lililonufaika hivyo tunahitaji kuwafikia viziwi wengi waishio vijijini ili nao waweze kutambua na kuchukua hatua," alisema Mwalwega.

Lilian Mwakitalima, mwanachama wa CHAVITA, alisema hawana elimu juu ya utambuzi wa bidhaa feki ikizingatiwa kuwa mikoa ya Mbeya na Songwe ni maeneo ya mipakani, hivyo baadhi ya bidhaa zinazoingizwa nchini ni feki.

Alisema elimu ya kutambua bidhaa feki kwa wajasiriamali viziwi itasaidia kubaini bidhaa zilizokidhi vigezo na ambavyo vimepigwa marufuku kwa ajili ya kulinda afya ya muuzaji na mtumiaji.

Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo kwa Viziwi Tanzania (TAMAVITA), Kelvin Nyema, alisema elimu ya utambuzi wa bidhaa feki ilianza kutolewa mkoani Tanga na kwamba lengo ni kufika katika kila mkoa ili kulisaidia kundi hilo kufanya shughuli zao kwa utulivu.

Nyema alisema Mkoa wa Mbeya ambao unapakana na nchi mbalimbali lazima udhibiti mipaka na elimu kwa jamii juu ya utambuzi wa bidhaa feki itolewe hususani kwa kundi la viziwi kwa sababu ya hali zao ni rahisi kuuziwa au kutumiwa.

Mkurugenzi wa Udhibiti Bidhaa Bandia kutoka FCC, Godfrey Mshana, alisema elimu ya utambuzi bidhaa feki imekuwa ikitolewa kwa makundi mbalimbali ya wajasiriamali na kwa kutambua umuhimu wa elimu hiyo waliamua kulifikia kundi la viziwi, ili kuongeza mapambano ya kudhibiti biashara hiyo.

Alisema tume imejikita katika kuhakikisha wananchi wanatumia bidhaa bora zilizokidhi vigezo kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali kudhibiti uingizwaji wa bidhaa bandia mipakani na kwa njia ya panya.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika, alisema serikali kupitia warajis wa vyama vya ushirika, imejitahidi kuhamasisha viziwi kujiunga kwenye vikundi ili kunufaika na mikopo ya halmashauri kwa masharti nafuu.

# UVCCM yataka vijana kuichagua CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIJANA wametakiwa kukiunga mkono Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho ndiyo chenye sera na ilani zilizowalenga kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa kuelekea hatua ya maendeleo na kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana CCM (UVCCM), Raymond Mwangwala, wakati akifunga kampeni za Jimbo la Mfenesini, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema Ilani ya uchaguzi ya CCM kwa upande wa Zanzibar, imelenga kutoa ajira 300,000 ambazo zitatokana na utekelezaji wa miradi ya kilimo, uvuvi wa bahari kuu pamoja na ujenzi wa viwanda vidogo.

Aliwataka vijana wasikubali kurubuniwa na vyama vingine vya upinzani ambavyo havina sera zilizojikita katika kuwaendeleza kiuchumi na kupambana na umaskini.

"Vijana msikubali kurubuniwa na wapinzani ambao hakuna chama chenye ilani iliyojikita na kuwainua kiuchumi isipokuwa Chama Cha Mapinduzi," alisema.

Alisema viongozi wa vyama vya upinzani wameshindwa kutengeneza chama kuwa na misingi imara na kwamba hawatoweza kuijenga serikali katika misingi bora itakayowaletea maendeleo wananchi.

Mgombea wa nafasi ya uwakilishi Jimbo la Mfenesini Unguja, Machano Othman Said, alisema akichaguliwa kuliongoza tena jimbo hilo ameweka malengo ya kutekeleza mambo matatu ya msingi ikiwamo usambazaji wa majisafi na salama, ajira kwa vijana na kinamama kwa kuwapatia mikopo pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya barabara za ndani.

Aliwataka wananchi wa jimbo hilo kujitayarisha na ujenzi wa stendi ya gari za abiria pamoja na soko la kisasa kwa nyanya na tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi utekelezaji wa mradi huo na kusaidia kuzalisha ajira zaidi kwa vijana.

"Nawaomba wananchi na wanachama wa Jimbo la Mfenesini kunichagua tena kuliongoza jimbo hilo, ambapo mambo muhimu ikiwamo usambazaji wa maji katika hatua ndogo zilizobakia tutatimiza ahadi yake," alisema.

Kwa upande wake mgombea wa Jimbo la Mfenesini kwa nafasi ya ubunge, Zubeida Khamis Shaibu, alisema akichaguliwa amejipanga kutatua kero za kinamama ikiwamo kuviwezesha vikundi vya wajasiriamali.

"Nikichaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mfenesini, nimejipanga kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili wanawake ikiwamo kuviwezesha vikundi vya wajasiriamali," alisema.

Aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Masoud Ali Khamis, aliwataka wapigakura na iliyokuwa timu yake ya uchaguzi kuelekeza nguvu zote kwa wagombea wa uchaguzi wa CCM kuwa wanashinda katika uchaguzi huo na kusubiri maendeleo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (katikati), akikata utepe kufungua jengo jipya la Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, huko Chakechake Pemba jana. Kulia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Salum Maulid Salum. **PICHA: IKULU**

# Viongozi wa dini waaswa kuchanganya dini na siasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa dini wametakiwa kutoichanganya dini na siasa na kusababisha uvunjifu wa amani na utulivu katika nchi hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Katibu wa Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, kufuatia kauli ya Katibu Mkuu wa Shuraa ya Maimamu Tanzania Bara, Sheikh Issa Ponda, aliyoitoa katika majukwaa ya kisiasa akisema maneno yaliyo kinyume na taratibu za kidini.

Akinukuu maneno ya sheikh huyo, alisema alipanda katika jukwaa la kisiasa na kusema kuwa Waislamu Watanzania wamekubaliana kumpa kura mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu na endapo waumini hao hawatampa kura mgombea huyo Mungu hatawaelewa na dua zao hazitakubaliwa, jambo ambalo ni kinyume na taratibu na maandiko ya dini.

Pia, alisema sheikh huyo alinukuliwa kutoa kauli za kuwataka waumini kutokukaa kimya endapo matokeo ya uchaguzi yatakuja kinyume na matarajio yao ya kisiasa jambo ambalo ni kinyume na taratibu za nchi.

Katibu wa Mufti alisema Ofisi ya Mufti Zanzibar, imesema haitambui makubaliano hayo na wala haikubali kauli hiyo na kuwataka viongozi wa dini kutochanganya dini na matakwa ya kisiasa ambayo ni kinyume na mwongozo wa vitabu vya dini na ni kitendo cha uchochezi na uvunjifu wa amani.

"Tanzania haikuanzisha mfumo wa vyama vya kisiasa kwa misingi ya kidini na mtazamo wa kwamba dua hazitokubaliwa na Mungu hatotuelewa ni upotoshaji wa kidini na mtazamo huo haukubaliki katika dini," alisema.

Alisema, kila raia ana uhuru wa kuchagua kiongozi anayemtaka ambaye anahisi atatekeleza mahitaji yake na kwa upande wa dini inawataka viongozi kuhubiri amani, usawa na upendo na kuacha kuhubiri mambo ambayo yatalea tofauti baina ya watu.

Alisema Sheikh Ponda si msemaji wa Waislam Tanzania, mwenye dhamana ya kusimamia Waislamu wote kwa Tanzania bara ni Mufti wa Tanzania Bara, Sheikh Abubakar Zubeir na kwa upande wa Zanzibar Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi.

Ofisi ya Mufti Zanzibar imewataka walimu wa madrasa kuwapa mapumziko wanafunzi wa madrasa zote kwa muda wa wiki moja kuanzia Oktoba 25, hadi Novemba 2, mwaka huu kutokana na harakati za uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu.

Aliwataka wazazi na walezi kuwadhibiti watoto wasizurure ovyo ili kuwaweka katika hali ya amani na kuwaepusha na vitendo viovu.

Pia Maimamu, Masheikh na Makatibu wa Zanzibar wametakiwa kuitumia Ijumaa kuiombea dua nchi ili ipate amani na ufanyike uchaguzi katika hali ya amani na usalama.

## Dk. Mwinyi aahidi ujenzi barabara Unguja Ukuu-Ngabwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema akichaguliwa kuwa rais atajenga barabara ya kutoka Unguja Ukuu mpaka Ngabwa ili kuwarahisishia shughuli za kimaendeleo wananchi wa vijiji hivyo.

Aliwahakikishia wananchi kusimamia ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 3.5 na daraja lake, ili kuwarahishia huduma zao za kujipatia maendeleo.

Akizungumza na wananchi wa vijiji vya Uzi na Ng'ambwa, Mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni mwendelezo wa kampeni zake za kukutana na makundi mbalimbali, alisema pia atajenga hospitali ya kisasa katika kijiji hicho ili huduma muhimu zitolewe katika kijiji hicho ikiwamo ya mama na mtoto.

Alisema serikali ya awamu ya nane atakayoiongoza italifanyia kazi suala hilo na hata huduma za upasuaji zinafanyike katika kijiji hicho.

Alisema, ni kweli kwamba kutokana na jiografia ya kijiji hicho kuzungukwa na bahari ni lazima kuwapo huduma muhimu hasa za hospitali.

"Kama kijiji ambacho kinahitaji kusaidiwa basi ni hiki hasa kutokana na mazingira yake yalivyo, mgonjwa hawezi kufika kwa haraka upande wa pili hivyo nitahakikisha hili nalifanyia kazi kwa nguvu zote," alisema.

Alisema ili kuwa na maendeleo katika eneo ni lazima kuwa na huduma muhimu ikiwamo miundombinu imara, daraja na barabara kwa kuwa kutokuwapo kwa mambo hayo huduma nyingi zinaathirika.

Akizungumzia watu wenye ulemavu aliwahakikishia kuendelea kuwasaidia katika kujiendeleza na kuwakomboa kimaisha katika shughuli zao za kujiletea maendeleo kupitia kituo chao katika kijiji hicho.

Pia, ahadi yake kwa wakulima wa mwani atahakikisha anawapatia zana za kisasa na kiwanda maalum cha zao hilo ili lipate soko la uhakika.

Dk. Mwinyi, alisema serikali ya awamu nane haitakuwa na huruma kwa watendaji ambao hawatokuwa tayari kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

"Nitakuwa wa kwanza kufatilia na katika serikali yangu itakuwa haina watendaji wa kukaa ofisini, watu wote watatembea ili kuwatumikia wananchi ndio lengo langu kuu la kugombea nafasi hii," alisisitiza.

Aliwasisitiza wananchi wa kijiji hicho kuachana na magendo na kutafuta njia nzuri za kuboresha maisha yao na kuachana na utumiaji wa dawa za kulevya.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdallah Juma Sadala 'Mabodi', alisema kijiji hicho kina historia kubwa kwa Afro Shirazi Party (ASP) katika kutafuta Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Alisema, kwa sasa ukombozi wa nchi umekwisha na uliobaki ni wa kimaendeleo kupitia Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 na kuwaomba wananchi wa kijiji hicho kuwachagua viongozi wa CCM ili waweze kuwaletea maendeleo.

Wananchi wa vijiji hivyo walisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kutokuwa na hospitali hivyo walimwomba mgombea huyo kuwajengea ili kutoa huduma zote hasa za kujifungua na kuwapatia elimu ya afya ya vijana ya huduma ya kwanza na kuwahudumia magonjwa ya hafla.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

IN THE RMS COURT / DISTRICT COURT OF MOSHI

AT MOSHI

MISC.CIVIL APPL NO.03 OF 2019

EVA ELILIMA MAWOLE........................................ PLAINTIFF/APPL.

VERSUS

BOSCO THADEI KOMBA................. DEFENDANT

NOTICE OF MENTION/HEARING

TO: BOSCO THADEI KOMBA.

Take Notice that the above case has been fixed for /hearing/mention/ruling/Judgement in the RMS court at Moshi on 26th the day of October 2020 at 9:00am Oclock in the forenoon.

You may appear in person or by advocate of agent dully authorized to do so and you are directed to produce on that day of document under which you intend to rely in support of your case.

TAKE FURTHER NOTICE that, default of your appearance on that day before mention the court will proceed with the matter in your absence.

A copy of the petition of appeal, Judgement and decree are attached hereto.

Given under my hand and seal of this Court this 16th day of October, 2020

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE I /C

MOSHI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROBINSON JOHN LIUNDI**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **FORESTER STATION WAGON** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 352 DUN.**

CHASSIS NAMBA **SH5010538.**

ENGINE NAMBA **EJ20D419722.**

YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLSI.

**TAARIFA YA POLISI: DAR/URA/RB/743389/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ESTHER JULIUS MASELE**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA HIACE** YENYE NAMBA ZA **USAJILI T604 BTM.**

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLSI.

**TAARIFA YA POLISI DOD/DOD/RB/731529/2020.**

215953602

## KUPOTEA KWA CHETI

**MARWA MAGEGU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2558-0009** kilichotolewa na **Baraza la Mitihani la Taifa** kupitia **SOMAGEDI SEKONDARI OCTOBA, 2012.**

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Control No: 9910818026639.**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;318/2020**

Ombi la **MARY SIMBO MUSHI** ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **PAULO MKANYAVANU MWANGAMILA.** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **24/11/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **21/10/2020.**

215953302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WINNIE GEORGE NZUNDA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI **AINA YA TOYOTA RAV4** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 867 DLX.**

CHASSIS NAMBA **ACA365013044.**

ENGINE NAMBA **2AZ2605138.**

YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**Control No: 9910819460873.**

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUPLIC TANZANIA**
**DODOMA DISTRICT REGISTRY**
**AT DODOMA**

Probate and Administration cause no .9 Of 2019
In the matter of the Estate of the late JOSEPH WAZIRI MAHENGE of Zahanati within Dodoma City.

And

In the matter of Application for letters of Administration by WITNESS AMULIKE MBILINYI

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**


ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 27 day of 10, 2020.

Dated at Dodoma this 20 day of 10, 2020.

DEPUTY REGISTRAR

## kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport)



**ZAKARIA MESIA MWAKIPESILE** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria **(Passport)** yenye namba **TAE 325051** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/694385/2020.**

21593802

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Buyoya ahukumiwa maisha jela mauaji ya Ndadaye

**BUJUMBURA, Burundi**

MAHAKAMA Kuu nchini Burundi imemhukumu kifungo cha maisha rais wa zamani wa nchi hiyo, Meja Pierre Buyoya baada ya kumkuta na hatia ya kumuua mrithi wake, Melchior Ndadaye mwaka 1993.

Hata hivyo, Buyoya (pichani) hakuwapo Burundi.



Mahakama hiyo ilisema katika tangazo la hukumu hiyo dhidi ya Meja Pierre Buyoya, kuwa kiongozi huyo wa zamani amepewa kifungo cha maisha jela kutokana na mchango wake katika mapinduzi ya kijeshi ya mwaka 1993 dhidi ya Rais Melchior Ndadaye.

Mahakama ilisema, Ndadaye alikuwa amekaa madarakani kwa miezi michache baada ya kumshinda Buyoya katika uchaguzi wa kwanza wa kidemokrasia kufanyika nchini Burundi, tangu nchi hiyo ilipopata uhuru wake kutoka ukoloni wa Kibelgiji mwaka 1962.

Hukumu hiyo iliyotangazwa kwenye mkesha wa kumbukumbu ya miaka 27 tangu kuuawa kwa Ndadaye, imewahusisha pia maofisa wengine waandamizi wa zamani 18, wakiwamo wawili waliokuwa Makamu wa Rais, Bernard Busokoza na Alphonse Marie Kadege.

Kama ilivyo kwa Buyoya, Busokoza na Kadege, wote wanaishi uhamishoni, na wamehukumiwa bila kuwapo mahakamani.

Kwa wakati huu, Pierre Buyoya ni mjumbe maalumu wa Umoja wa Afrika nchini Mali na katika ukanda wa Sahel, licha ya kuwekewa na nchi yake waranti ya kimataifa ya kukamatwa, tangu Novemba 2018. Mrithi wa Rais Melchior Ndadaye, Cyprien Ntaryamira, aliuawa pia miezi michache baada ya kuchukua madaraka, alipokuwa akisafiri katika ndege moja na rais wa zamani wa Rwanda Juvenal Habyarimana, ambayo ilidunguliwa katika anga la mji mkuu wa Rwanda Kigali, Aprili 6, 1994, na kuwaua wote waliokuwamo.

Tukio hilo lilifuatiwa na umwagaji mkubwa wa damu nchini Rwanda, uliogeuka mauaji ya kuangamiza dhidi ya watu wa jamii ya Watutsi, takribani milioni moja walipoteza maisha. Meja Pierre Buyoya mwenyewe hajatamka lolote baada ya hukumu hiyo.

***DW***

# Mchumba wa Jamal Khashoggi amshtaki mwanamfalme Saudia

**WASHINGTON, Marekani**

MCHUMBA wa mwandishi wa Saudia, Jamal Khashoggi, aliyeuawa nchini Uturuki, amewasilisha kesi mahakamani dhidi ya mwanamfalme wa Saudia, akimtuhumu kwa kuagiza mauaji hayo.

Hatice Cengiz na makundi ya wanaharakati ya haki za kibinadamu yalioanzishwa na Khashoggi kabla ya kifo chake, yanamshtaki mwanamfalme Mohammed bin Salman na zaidi ya watu wengine 20 kwa kiwango cha uharibifu kisichojulikana.

Khashoggi aliuawa na kundi la mawakala wa Saudia wakati wa ziara yake katika ubalozi wa Saudia mjini Instabul, Uturuki 2018.

Mwanamfalme huyo amekana kutekeleza mauaji hayo.

Khashoggi alikuwa mkosoaji mkubwa wa serikali ya Saudia na alikuwa akiishi mafichoni nchini Marekani, mara kwa mara akiliandikia gazeti la The Washington Post.

Katika kesi hiyo iliowasilishwa mjini Washington siku ya Jumanne, raia wa Uturuki bi Cengiz, anadai kuathiriwa binafsi na kifedha kufuatia kifo cha Khashoggi.

Kundi la kupigania haki za kibinadamu la, Democracy for the Arab World Now (Dawn), linasema kwamba operesheni zake ziliathirika.

Mashtaka hayo yanadai kwamba Khashoggi aliuawa "kufuatia maagizo kutoka kwa mshukiwa Mohammed bin Salman".

"Lengo jingine la mauaji hayo lilikuwa wazi - kumzuia bwana Khashoggi kupigania mabadiliko ya kidemokrasia katika ulimwengu wa Waarabu akiwa nchini Marekani," ilisema kesi hiyo.

Katika mkutano uliofanyika kupitia video jana, mawakili wa Cengiz na Dawn, walisema lengo la kesi hiyo ni kuilazimu mahakama ya Marekani kumwajibisha mwanamfalme huyo kwa mauaji hayo na kupata stakabadhi zinazoonyesha ukweli, kulingana na gazeti la The Washington Post.

"Jamal aliamini kwamba kila kitu kinawezekana Marekani na sasa naweka imani yangu chini ya mfumo wa mahakama ili kupata haki na uwajibikaji," Cengiz alisema katika taarifa yake.

Jamal Khashoggi ni mwandishi maarufu aliyeangazia taarifa kubwa kwa mashirika tofauti nchini Saudia.

Aliunda urafiki na Osama bin Laden katika miaka yake ya kwanza alipoanza kuwa mwandishi wa habari na alifahamika kama mzalendo maarufu wa Saudia aliyelazimika kutoroka nchi hiyo.

Kabla ya kutoweka kwake katika ubalozi wa Saudia mjini Istanbul, uhamisho wa kibinafsi wa Khashoggi ulimlazimu kuishi Marekani, Uingereza na Uturuki.

***BBC***


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA**

## TAARIFA KWA UMMA

**TAREHE RASMI YA KUANZA MATUMIZI YA MFUMO WA STEMPU ZA KODI ZA KIELEKTRONIKI (ETS) KWA BIDHAA KAMA JUISI, MAJI YA KUNYWA, NA KAZI ZA FILAMU NA MUZIKI (CD/VCDS/DVD/KANDA ZILIZOREKODIWA)**

**Dar es Salaam, 21 Oktoba, 2020**

Kwa kuzingatia **Kanuni ya 29 ya Kanuni za Stempu za Kodi za Kielektroniki za Mwaka 2018** (yaani, "Kanuni"), Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") inapenda kuwafahamisha wazalishaji wote wenye leseni, waingizaji waliosajiliwa, wasambazaji, wauzaji wa bidhaa zinazotozwa kodi ya ushuru wa bidhaa, na umma kwa ujumla kwamba, tarehe 1 Novemba 2020 itakuwa ni tarehe rasmi ya kuanza matumizi ya Mfumo wa Stempu za Kodi za Kielektroniki (ETS) kwa juisi za matunda na mbogamboga, maji ya kunywa ya yaliyofungashwa kwenye chupa, na bidhaa za filamu na muziki (yaani, CD/VCDs/DVD/Kanda zilizorekodiwa).

Hatua hii inafuatia kukamilika na kuanza kwa matumizi ya mfumo huu kwa Awamu ya I na Awamu ya II kwa bidhaa za sigara, mvinyo, pombe kali, bia, na aina zote za vileo hapo mnamo tarehe 15 Januari 2019 na kwa bidhaa za vinywaji laini mnamo tarehe 1 Agosti 2019, mtawalia.

Kutokana na ufafahanuzi wa hapo juu, na kwa mkutadha wa kutekeleza matakwa ya Kifungu cha 5(1)(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, SURA 399 R.E 2019, wadau wote pamoja na umma kwa ujumla wanataarifiwa kuwa juisi, maji ya kunywa yaliyofungashwa kwenye chupa, kazi za filamu (kwa mfano, CDs/VCDs/DVDs/Kanda zilizorekodiwa), zitakazozalishwa ama ndani ya nchi au kuingizwa kutoka nje ya Jamhuri ya Muungano, kwamba kuanzia mnamo tarehe 1 Novemba 2020 lazima bidhaa tajwa ziwe zimebandikwa Stempu za Kodi za Kielektroniki kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 4 ya Kanuni.

Na kwa kuwa bidhaa hizi hazikuwa zikibandikwa stempu hapo awali, hivyo basi, bidhaa zote zilizopo sokoni na kwenye maghala ya watengenezaji au waingizaji wa bidhaa hizo, ambazo hazijabandikwa stempu za kodi za kielektroniki, zinaruhusiwa kuendelea kuuzwa kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu (3), yaani, ama kabla au hadi kufikia mnamo tarehe 31 Januari 2021, kama ilivyofafanuliwa kwenye Kanuni ya 44(3) ya Kanuni tajwa. Baada ya tarehe hiyo, bidhaa hizi zote hazitaruhusiwa kuwepo sokoni bila kubandikwa Stempu za Kodi za Kielekroniki.

Hivyo, kila mzalishaji au muingizaji wa bidhaa tajwa anapaswa kutoa taarifa TRA juu ya idadi ya bidhaa alizonazo ambazo hazijabandikwa stempu za kodi za kielektroniki kabla ya tarehe rasmi ya kuanza matumizi ya mfumo huu kwa kujaza fomu maalum inayopatikana kwenye ofisi za TRA za kila Mkoa na katika tovuti ya Mamlaka (www.tra.go.tz). Aidha, TRA inawakumbushwa wafanyabishara na wadau wote kuwasilisha taarifa kamili ya chapa zao (brands) na idadi ya stempu za ETS wanazokusudia kutumia kwa mwaka ujao ili waweze kusajiliwa katika Mfumo wa Usimamizi wa Stempu za Kodi za Kielektroniki (ETSMS) na kuweza kuagiza stempu kupitia tovuti salama (https://taxstamp.tra.go.tz/) iliyofungamanishwa ndani ya tovuti ya Mamlaka.

Kwa maelezo na ushauri zaidi, TRA inawahimiza wazalishaji, wafanyabiashara, waingizaji, na wadau wote kutembelea Ofisi za TRA kote nchini, tovuti yetu (www.tra.go.tz), au Kituo cha Huduma kwa Mteja kinachopatikana kwa namba za kupiga bure 0800 750 075 au 0800 780 078, namba ya WhatsApp 0744 233 333, au barua pepe services@tra.go.tz.

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Dr. Edwin P. Mhede, Ph.D.**
**KAMISHNA MKUU**

# MESSI AWEKA REKODI



**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi alifunga bao moja na kuweka rekodi ya kufunga mwanzo wa msimu mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya 16 mfululizo.

Pia Pedri mwenye umri wa miaka 17, akifunga bao lake la kwanza kwa timu ya wakubwa, wakati Barcelona ikiifunga Ferencvaros mabao 5-1.

Messi alifunga kwa mkwaju wa penalti na kuipa Barca uongozi kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Camp Nou.

Ansu Fati alifunga bao la pili kwa Barca, huku Philippe Coutinho akiongeza la tatu.

Gerard Pique alitolewa kwa kadi nyekundu baada ya kumchezea faulo Ihor Kharatin na kuzawadiwa penalti, kabla ya Pedri na Ousmane Dembele kufunga bao la nne na la tano kwa Barca.

Messi sasa amejiwekea rekodi ya kufunga katika kila mwanzo wa msimu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa huu ni msimu wake wa 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kufanya hivyo.

Baada ya mchezo huo, Koeman alisema mchango wa Messi, ambaye alitaka kuondoka klabuni hapo kipindi cha majira ya joto kilichopita, ulikuwa mkubwa mno kwa klabu hiyo.

# TUCHEL: TUMECHEZA VIBAYA DHIDI YA UTD

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA Mkuu wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, ameelezea kipigo cha mabao 2-1 cha Jumanne kutoka kwa Manchester United kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ni kibaya zaidi kwa klabu hiyo.

Marcus Rushford aliifunga PSG zikiwa zimebaki dakika tatu mpira kumalizika na kuipa ushindi Man United kwenye mchezo wake huo wa kwanza wa Kundi H jijini Paris.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, PSG, walikuwa bila Marquinhos na Marco Verratti na United wakawa na faida wakianza kupata bao kupitia kwa Bruno Fernandes aliyefunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 23.

Licha ya mshambuliaji wa 'Mashetani Wekundu' hao, Anthony Martial kujifunga, lakini United wakaondoka na ushindi huo muhimu.

"Kipindi cha kwanza hatukuwapo kabisa mchezoni," alisema Tuchel akiiambia beIN SPORTS.

"Sijui kwa nini, lakini naweza tu kusema kwamba, hatukuwa kwenye kiwango chetu na tulishindwa kabisa kurudi mchezoni.

"Kwa kweli huu ndio mchezo mbaya zaidi kwetu, kupoteza nyumbani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mchezo wa kwanza ni gharama kubwa."






# LAMPARD AWASIFU MENDY, THIAGO

**LONDON, England**

FRANK Lampard alisifia ulinzi imara wa Thiago Silva na Edouard Mendy wakati Chelsea ikitoka sare ya bila kufungana na Sevilla kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

'Blues' hao katika mchezo wao uliopita waliruhusu kufungwa mabao matatu na Southampton kwenye Ligi Kuu ya England pale Stamford Bridge na kutoka sare ya 3-3.

Lakini katika mchezo wa juzi Jumanne, walionekana kubadilika na safu yao ya ulinzi ilikuwa imara zaidi kuzuia mashambulizi ya hatari kwenye mechi hiyo ya Kundi E.

Lampard alifanya mabadiliko matatu kwenye safu yake ya ulinzi tofauti na ile ya Jumamosi, akimwanzisha Reece James kama beki wa kulia, Mendy golini na Silva kama mlinzi wa kati.

Baada ya mchezo huo, Lampard aliisifia safu yake hiyo ya ulinzi na kusema imeonyesha mchango mkubwa kwenye mchezo huo.

"Ni kitu ambacho unapenda kukiona, kwani mambo yalikuwa tofauti kabisa," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Thiago alionyesha vitu fulani tofauti na kwa uhakika uzoefu wake ulionekana wazi kabisa.

"Mendy pengine ndiye aliyefanya kazi ya ziada kuokoa moja ya hatari kubwa langoni mwetu, kwa hakika walionyesha tofauti kubwa sana."




# SOLSKJAER

## AFUNGUKIA USHINDI KWA PSG

**PARIS, Ufaransa**

OLE Gunnar Solskjaer, amesema Manchester United walistahili ushindi usiku wa kuamkia jana dhidi ya PSG kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakiicha mabao 2-1.

Mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Parc des Prinnces na mabao yote matatu yalifungwa na wachezaji wa timu ya Man United.

Bruno Fernandes alianza kufunga bao la kwanza dakika ya 23 kwa mkwaju wa penalti likisawazishwa na Anthony Martial aliyejifunga dakika ya 55 na nyota wa mchezo huo Marcus Rashford alifunga bao la ushindi dakika ya 87.

Solskjaer ambaye alianzisha kikosi chake bila nahodha Harry Maguire huku akimweka pia benchi kiungo Paul Pogba, amesema anahisi vizuri kwa timu yake kushinda na walistahili kupata ushindi huo.

"Najihisi vizuri na nina furaha kwa timu kushinda, wachezaji wote walitambua kwamba wana kazi ngumu ya kufanya na hawajaniangusha, wanastahili pongezi katika hili," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Vijana walipambana kwa dakika zote 90, tulistahili ushindi huu kwa sababu tulicheza vizuri na kila nafasi tuliyoipata tuliitumia vizuri na hatimaye tukashinda."

Man United ilikwenda kwenye mchezo huo ikitoka kushinda mabao 4-1 dhidi ya Newcastle United katika mechi ya Ligi Kuu ya England.

## OZIL SASA ATOSWA MAZIMA ARSENAL

**LONDON, England**



SASA ni rasmi kwamba, kiungo Mesut Ozil ametoswa na klabu yake ya Arsenal baada ya jina lake kutojumuishwa katika kikosi cha wachezaji wa timu hiyo watakaoitumikia kwenye Ligi Kuu.

Huku akiwa analipwa mshahara mkubwa zaidi, Ozil amekuwa na maisha magumu kwenye kikosi cha Arsenal tangu kuondoka kwa Arsene Wenger.

Wenger alimnunua Ozil kwa dau lililoweka rekodi klabuni hapo akitokea Real Madrid, lakini tangu kuondoka kwake hapo kwenye dimba la Emirates, amekuwa hana nafasi ya kucheza.

Alianza kwa kuwekwa pembeni kwenye orodha ya wachezaji watakaoshiriki Ligi ya Europa, ambapo hakuweza kupenya kwenye kikosi cha wachezaji 25.

Na juzi Jumanne, Ozil hakuwekwa kwenye kikosi cha wachezaji 25 watakaoshiriki Ligi Kuu England.

Kwa mujibu wa ESPN, jina la Ozil mwenye umri wa miaka 32, halipo kwenye orodha ya wachezaji wa Arsenal.

Kwa mujibu wa kanuni za Ligi Kuu England zinazitaka klabu kuwasilisha majina 25 ya wachezaji wake, ambapo kati yao 17 ni lazima wawe wazawa wa Uingereza na hapo ndipo Ozil alipokatwa rasmi.



## FLICK AHOFU UBORA BAYERN KUSHUKA

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Bayern Munich, Hansi Flick, amesema ni vigumu kwa timu hiyo kubaki katika kiwango cha juu kama msimu uliopita.

Bayern Munich jana walianza kibarua kizito cha kuikabili timu yenye ushindani mkubwa Atletico Madrid katika michuano hiyo kwenye Kundi A.

Bayern walilazimika kupunguza siku za maandalizi ya msimu mpya baada ya kuwa na siku takribani 26 tangu walipocheza mechi ya fainali ya Ligi Mabingwa dhidi ya Paris St-Germain.

Bayern walishinda pia taji la Ligi Kuu nchini Ujerumani na Kombe la Ligi na kushinda jumla ya mataji matatu, ingawa majina makubwa baadhi yao yameondoka kama vile Thiago Alcantara na Phillipe Coutinho.

"Itakuwa vigumu kuwa tulivyokuwa msimu uliopita, kila timu imeimarika zaidi msimu huu licha ya mapungufu ambayo huwa hayakosekani kwenye timu," alisema Flick ambaye alicheza mechi hiyo ya kwanza Ligi ya Mabingwa Ulaya bila uwapo wa majeruhi Leroy Sane na Tanguy Nianzou.

"Tulikuwa na wiki moja pekee ya maandalizi, lakini hivi sasa angalau nimeridhika, wiki moja haitoshi, lakini nafurahi kwa sababu sina majeruhi wengi," aliongeza kocha huyo.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE SASA ATAKA KUJIUNGA NA LIVERPOOL

Kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na kwenda kujiunga na Real Madrid, lakini sasa nyota huyo...

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa Klabu ya Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe anavutiwa zaidi na kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool, kwa mujibu wa gazeti la Le Parisien.

Kwa muda mrefu, mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain, amekuwa akitajwa kuelekea kule Hispania kwa miamba wa ligi hiyo, Klabu ya Real Madrid.

Hata hivyo, sasa Mbappe inaaminika kwamba anataka kuondoka pale Parc des Princes haraka iwezekanavyo, lakini safari yake ni kule Liverpool katika dimba la Anfield.

Mbappe ana mkataba na PSG hadi mwaka 2022, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa amripotiwa kwamba hana mpango wa kuongeza muda wa kuendelea kukaa hapo jijini Paris.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018, alielezea kwamba, Liverpool ndio timu anayopenda kwenda kucheza na ni shabiki wake namba moja.

Kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na kwenda kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Real Madrid, lakini sasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, akili yake ipo Liverpool.

Gazeti la Le Parisien limeripoti kwamba, Mbappe anavutiwa zaidi na staili ya uchezaji ya Liverpool kuliko ile ya Real Madrid.

"Ni wazi kwamba, sasa safari yake ni Liverpool, anaonyesha hana nia ya kwenda Real Madrid," gazeti la Le Parisien limemnukuu mtu wa karibu na Mbappe.

Kocha mkuu wa Real Madrid ambaye ni Mfaransa mwenzake, Zinedine Zidane, hajaficha namna anavyotaka nyota huyo kuwa kwenye kikosi chake.

Wapinzani wa Real Madrid kwenye soka la Hispania, Barcelona pia wameripotiwa kuiwinda saini ya mchezaji huyo.

## KWA UFUPI

**MARTESACKER AMFUNGUKIA OZIL**

MLINZI wa zamani wa Arsenal, Per Mertesacker, anaamini kiungo, Mesut Ozil kwa sasa mawazo yake hayapo tena kwenye soka, baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, kuachwa kwenye kikosi cha 'Washikabunduki' hao cha Ligi Kuu, juzi Jumanne. ***(Klick and Rush podcast via Mail)***

**WHITE AWINDWA LIVERPOOL**

LIVERPOOL inaweza kumshawishi, mlinzi wa Brighton, Ben White mwenye umri wa miaka 23, au mlinzi wa Uturuki na Schalke, Ozan Kabak, mwenye umri wa miaka 20, kuziba pengo la Mholanzi, Virgil van Dijk, 29. ***(TV 2)***

**SPURS KUMFUNGA ZAIDI SON**

KLABU ya Tottenham Hotspur wapo mbioni kuingia mkataba mpya wa muda mrefu na mshambuliaji wa Korea Kusini, Son Heung-min, mwenye umri wa miaka 28. ***(The Athletic)***

**RIO AMTETEA SOLSKAJAER**

RIO Ferdinand anaamini Ole Gunnar Solskjaer amesikitishwa na jinsi bodi ya timu hiyo ilivyoshindwa kufikia malengo yake kwenye usajili kipindi cha majira ya joto kilichopita. ***(Mail)***

**SPURS, FERNANDES KUACHANA**

KLABU ya Tottenham inafikiria kumrejesha Gedson Fernandes mwenye umri wa miaka 21 kwenye klabu yake ya Benfica katika dirisha lijalo la usajili. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno alijiunga na Spurs kwa mkopo wa miezi 18 Januari. ***(A Bola)***

**SARR, DEENEY WAJIFUNGA**

MWENYEKITI na Mtendaji Mkuu wa Watford, Scott Duxbury, amesema winga wa kimataifa wa Senegal, Ismaila Sarr, mwenye umri wa miaka 22, na Muingereza Troy Deeney, 32, wamejifunga na klabu hiyo. ***(London Standard)***

**PEREIRA AJIPA MATUMAINI**

MLINZI wa kulia wa Ureno, Ricardo Pereira, mwenye umri wa miaka 27, ambaye amefanyiwa upasuaji wa goti, ana matumaini atarudi tena kuichezea Leicester City ndani ya wiki sita zijazo. ***(O Jogo, via Independent)***

**BARCA YAKWAMA KWA GARCIA**

MANCHESTER City imekataa ofa ya dau la pauni milioni 15.4 na marupurupu kutoka kwa Klabu ya Barcelona ili kumnunua beki, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho. ***(Sky Sports)***

**RICHARLSON NA SMS 10,000**

MSHAMBULIAJI wa Everton, Richarlison, amesema alipata ujumbe mfupi 10,000 kupitia WhatsApp ndani ya dakika tano baada ya mchezaji mwenzake wa Brazil, Neymar kuonyesha namba yake kwenye 'gemu ya video'. ***(Star)***

**13 WA AZ WAPATA CORONA**

KLABU ya AZ Alkmaar imesema wachezaji wake 13 wamekutwa na maambukizi ya virusi vya corona, lakini mchezaji wao wa leo Alhamisi wa Ligi ya Europa dhidi ya Napoli utaendelea kama ulivyopangwa. ***(Mail)***

**GRIEZMAN KUONDOKA BARCA**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 29, yupo tayari kupunguza mshahara wake ili aondoke klabuni hapo na kujiunga na klabu nyingine. ***(Marca)***

**JUVE, RONALDO WALAUMIWA**

WAZIRI Vincenzo Spadafora, ameishutumu Juventus na mshambuliaji wao wa Ureno, Cristiano Ronaldo, kurudi Italia baada ya kukutwa na virusi vya corona. ***(Gazzetta dello Sport)***

**UNITED YAMFUATILIA GOMES**

KLABU ya Manchester United inamlenga kiungo wa kati wa Sporting Lisbon mwenye umri wa miaka 16, Luis Gomes. Kiungo huyo raia wa Ureno amepewa jina la utani la 'Luis Figo' ajaye nchini humo. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA YAITISHA YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Polisi Tanzania, Ally Suleiman, amesema wanahitaji kuendeleza rekodi nzuri dhidi ya Yanga katika mechi yao ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Suleiman alisema tangu msimu uliopita wamekuwa wakiipa wakati mgumu Yanga na wamejipanga kuondoka na ushindi katika mechi ya leo.

Suleiman alisema wamejipanga vizuri na wana imani na wachezaji wao watapambana ili kutochafua rekodi waliyonayo dhidi ya vigogo hao wa soka nchini.

"Hatuna hofu na majina ya wachezaji wao wa kigeni, hatuhofii chochote, tumejipanga vizuri, ila tunawaheshimu wapinzani wetu kwa kuwa ni wakongwe katika ligi," Suleiman alisema.

Aliongeza msimu huu wamejipanga kuondoka na ushindi kwa sababu matokeo ya sare si mazuri tena.

"Hawajawahi kupata pointi tatu kutoka kwetu, msimu huu tunahitaji ushindi na hilo linawekezana," aliongeza.

Polisi Tanzania itaivaa Yanga ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Gwambina FC kwenye Uwanja wake wa nyumbani wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Katika msimamo wa ligi, Yanga yenye pointi 13 iko katika nafasi ya tatu baada ya kucheza mechi tano wakati Polisi Tanzania ambayo imeshuka dimbani mara sita, ina pointi 11 na iko katika nafasi ya saba.

Mshambuliaji wa Yanga, Ditram Nchimbi akiwa na Polisi Tanzania msimu uliopita, alifunga hatrick-trick katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyomalizika kwa sare ya mabao 3-3 dhidi ya timu hiyo yake ya sasa.

## Kada wa CCM amkubali Samatta

**Na Mwandishi Wetu**

KADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na mdau wa soka hapa nchini, Mohamed Noray 'Mo Noray', amempongeza nahodha wa timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, ambaye sasa anakipiga katika klabu ya Fenerbahçe inayoshiriki Ligi Kuu Uturuki kwa kuendelea kulitangaza vema jina la Tanzania kwenye ya medani ya soka.

Mdau huyo alisema hayo jana wakati wa kutoa maoni yake juu ya kumbukizi ya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Nyerere na kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Mo Noray ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Ujenzi Tanzania Works Building Limited, ambayo inakarabati Uwanja wa Ndani wa Taifa, alisema anamkumbuka Mwalimu Nyerere namna alivyoipa kipaumbele sekta ya michezo, hivyo Watanzania wanatakiwa kuendelea kumwenzi kiongozi huyo ili michezo ifanye vizuri.

Alisema Mwalimu Nyerere alikuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha vijana kuithamini michezo hapa nchini na kupitia mafanikio ya Samatta, vijana wengi watajituma ili kuipeperusha vema bendera ya nchi katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Alisema licha ya idadi ya Watanzania kukaribia milioni 55, bado Samatta amekuwa mchezaji pekee katika karne hii ambaye amewatoa kimasomaso Watanzania kwa kucheza ligi ngumu barani Ulaya, ikiwamo Aston Villa ya Ligi Kuu England na Fenerbahçe ya Uturuki.

"Kiukweli nampongeza sana Samatta ametuletea sifa taifa letu kujulikana barani Ulaya kutokana na juhudi zake binafsi alizozifanya mpaka kufikia alipo, hivyo ni vema tukampa sapoti kwa hali na mali kuhakikisha Watanzania wapo nyuma yake," alisema Mo Noray.

Aliwataka wadau mbalimbali wa soka nchini kujitokeza kujenga viwanja vya michezo ili kutengeneza vipaji zaidi vya wanamichezo.

Kuhusu uchaguzi mkuu, mdau huyo alisema enzi za uhai wa Mwalimu Nyerere, alipenda kuhubiri amani, hivyo anawakumbusha Watanzania kwenda kupiga kura kwa amani na kumchagua rais atakayelifikisha taifa katika mtazamo wa kimataifa, ambaye ni mgombea wa CCM, Dk. John Magufuli.

CHA PILI...




Mshambuliaji wa Azam FC, Iddi Suleiman 'Nado', akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Ihefu FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Sokoine juzi. Bao la kwanza lilifungwa na Ayoub Lyanda, yote yakitengenezwa na Prince Dude. **MPIGAPICHA WETU**

## Amri aikana Mbeya City

**Na Adam Fungamwango**

HUKU akiiongoza Mbeya City kufunga bao lake la kwanza msimu huu, uongozi wa klabu hiyo umetangaza rasmi kusitisha mkataba wake na Kocha Mkuu, Amri Said, lakini akifunguka kuwa hakuna makubaliano yoyote waliyofikia na waajiri wake hao kutokana na utaratibu uliotumika kuusitisha.

Mbeya City ilikubali kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Mwadui FC kwenye Uwanja wa Mwadui Complex mjini Shinyanga juzi, huo ukiwa ni mwendelezo wa klabu hiyo kufanya vibaya, hatua ambayo uongozi wa klabu hiyo iliamua kumsitishia mkataba.

Katibu Mkuu wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe, alisema katika taarifa yake kuwa klabu hiyo imefikia uamuzi huo baada ya majadiliano ya pande mbili kutokana na mwenendo usioridhisha wa timu hiyo kwenye Ligi Kuu Bara inayoendelea.

Kimbe alisema katika kipindi cha mpito, timu hiyo itakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Mathias Wandiba.

Hata hivyo, Amri aliliambia gazeti hili hajafanya mazungumzo na hajafikia makubaliano yoyote na uongozi wa klabu hiyo, ila anawataka wampe barua ya kumfukuza kazi na si vinginevyo.

"Awali waliniambia tukaandikishiane kusitisha mkataba, lakini wakanitaka mimi niandike nimejiuzulu, nikakataa, nikawaaambia kama wao wanaona tatizo ni kocha, basi waniandikie barua ya kuniondoa kwa kufuata taratibu za kazi," alisema Amri.

## Uchaguzi Lindi mambo yameiva

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI wa Chama cha Soka Mkoa wa Lindi (LIREFA), umepangwa kufanyika Novemba 18, mwaka huu mkoani humo, imeelezwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Karume Benjamin, alisema uchaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa Katiba ya LIREFA.

Karume alisema fomu kwa ajili ya wadau wanaotaka kuwania nafasi mbalimbali zilianza kutolewa jana hadi Oktoba 26, mwaka huu na mchakato wa kuchuja wagombea utafanyika baada ya kukamilika kwa mchakato huo wa awali.

Alisema kamati itapokea pingamizi kati ya Oktoba 30 hadi Novemba Mosi, wakati Novemba 8 na 9, mwaka huu watapokea rufani na siku inayofuata zitasikilizwa.

"Uchaguzi huu ni kwa mujibu wa katiba, ikumbukwe kipindi cha miaka minne kitakapomalizika, basi maandalizi ya uchaguzi mwingine hufuata," alisema Wakili Karume.

Tayari Chama cha Soka cha Wanawake Mkoa wa Lindi kimeshafanya uchaguzi wake na Alice Choaji amechaguliwa kuwa mwenyekiti, Aisha Mshana ametetea nafasi yake ya ukatibu.

Michezo
Alhamisi Oktoba 22, 2020
Nipashe



MBAPPE SASA ATAKA KUJIUNGA NA LIVERPOOL HABARI UK 22



Mshambuliaji wa PSG, Neymar, akikwepa kihunzi dhidi ya mabeki wa Manchester United, Scott McTominay (kushoto) na Aaron Wan-Bissaka katika mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa kwenye Uwanja wa Le Parc des Princes, Ufaransa, usiku wa kuamkia jana na United kushinda kwa mabao 2-1. **HABARI UK. 21**

# MAKOCHA SIMBA, YANGA WATEMA 'UPUPU' LIGI KUU

●●●Ni kuelekea mechi zao za leo wakizivaa Prisons na Polisi Tanzania, kila mmoja aeleza...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI vigogo vya soka nchini vikitarajiwa kushuka dimbani kwenye viwanja viwili tofauti hapa nchini kuwania pointi tatu muhimu, mabingwa watetezi, Simba wakiwa ugenini kuwakabili Prisons mjini Sumbawanga huku Yanga ikiwakaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, makocha wa timu hizo wametema 'upupu' kuelekea mechi hizo.

Simba na Yanga zenye pointi 13 kila moja, zinahitaji kuvuna pointi tatu katika mechi zao za leo ili kuifukuza Azam FC yenye pointi 21, na ndio vinara wa ligi hiyo, lakini ikiwa mbele mechi mbili zaidi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Suleiman Matola, alisema mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani kwa sababu wanakutana na moja ya timu bora kwenye Ligi Kuu Bara.

Matola alisema wamewaandaa wachezaji wao kucheza kwa nidhamu na kuongeza umakini kutokana na wapinzani wao kuwa na kikosi chenye nyota wazoefu na wanaojua 'kuusoma' vema mchezo.

Kiungo huyo wa zamani wa Wekundu wa Msimbazi, alisema kwao kila mechi ni ngumu na hiyo inawasaidia kuwajenga wachezaji kuelekea katika mashindano ya kimataifa na kuhakikisha wanatetea tena taji hilo.

"Mara zote tunapokutana na Tanzania Prisons tunakuwa na mchezo mgumu, ni timu ngumu, ila sisi pia tuko vizuri, tumejipanga kuonyesha ubora wetu, kikubwa ni kutumia nafasi tutakazotengeneza, Prisons ni timu inayosaka ushindi pia," Matola alisema.

Hata hivyo, katika mechi ya leo, Simba itamkosa nahodha wake, John Bocco, Paschal Wawa na kiungo, Clatous Chama ambaye bado hajarejea nchini.

Kocha Mkuu wa Prisons, Adolph Rishard, aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na wamejiandaa kucheza kwa nidhamu.

Rishard alisema wamefanya maandalizi yanayostahili na wanaupa umuhimu sawa na michezo mingine iliyopita kwa sababu dhamira yao kila wanapoingia uwanjani ni kuondoka na ushindi.

"Mpira una matokeo matatu, ingawa kila mwalimu anawaza kwanza ushindi, hakuna ambaye anaingia uwanjani akiamini anashinda, kwa sababu hiyo nimewaandaa wachezaji wangu kwenda kuwania pointi tatu, nimewataka wasicheze na jina la timu, wapambane na wachezaji wenzao watakaopangwa," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema hatarajii kufanya mabadiliko makubwa kutoka katika kikosi cha kwanza ambacho kimekuwa kikitumika kwenye mechi zilizopita na kuiwezesha timu hiyo kushinda michezo minne na sare moja kati ya mitano waliyocheza hadi sasa.

Alisema anachokifanya kwa sasa ni kukiongezea mbinu na hata kama kutakuwa na mabadiliko yatakuwa machache kulingana na hali ya wachezaji itakavyokuwa.

"Ninataka timu icheze pasi za haraka na kushambulia kwa kasi zaidi ili kutokutoa nafasi kwa wapinzani kupanda kutushambulia, hilo ndilo soka ninalolipendelea," alisema kocha huyo raia wa Burundi aliyerithi mikoba ya Mserbia Zlatko Krmpotic.

Alisema hana wasiwasi na uwezo wa wachezaji waliosajiliwa na timu hiyo na zaidi kikosi kilichokuwa kikianza kutokana na kuipa matokeo mazuri hadi sasa.

Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema kikosi chao kiko kamili kuwakabili Polisi Tanzania na msimu huu wamejipanga kuchukua pointi zote sita kutoka kwa 'Maafande' hao.

"Nikutake mwanachama, shabiki ujitokeze kushuhudia mchezo huu, umwonyeshe mwalimu Cedric Kaze tumemkubali katika timu yetu," Nugaz alisema.

Mechi ya leo itakuwa ni ya kwanza kwa Kaze ambaye amerithi mikoba iliyoachwa na Krmpotic katika kikosi hicho ambacho kina kiu ya kulikosa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu mitatu mfululizo.

Yanga inashuka dimbani pia ikiwa na rekodi ya kuwa na ukuta bora, imeruhusu bao moja katika mechi zake tano walizocheza wakati Simba na Azam zenyewe zimeruhusu  mabao mawili kila moja.



## MESSI AWEKA REKODI UEFA

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi alifunga bao moja na kuweka rekodi ya kufunga mwanzo wa msimu mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya 16 mfululizo.

Pia Pedri mwenye umri wa miaka 17, akifunga bao lake la kwanza kwa timu ya wakubwa, wakati Barcelona ikiifunga Ferencvaros mabao 5-1. **INAENDELEA UK. 20**



## POLISI TANZANIA YAITISHA YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Polisi Tanzania, Ally Suleiman, amesema wanahitaji kuendeleza rekodi nzuri dhidi ya Yanga katika mechi yao ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Suleiman alisema tangu msimu uliopita wamekuwa wakiipa wakati mgumu Yanga na wamejipanga kuondoka na ushindi katika mechi ya leo.

**INAENDELEA UK. 23**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002